JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# RASIMU YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

DESEMBA 2024

# JEDWALI LA YALIYOMO


UTANGULIZI ..... 4
DIRA ..... 6
**Msingi wa Dira** ..... 10
**Utawala, Amani, Usalama na Utulivu** ..... 10
1.1 Utangulizi ..... 10
1.2 Lengo ..... 10
1.3 Maeneo Yatakayozingatia ..... 10
1.3.1 Utawala Bora na Haki ya Jamii ..... 10
1.3.2 Serikali za Mtaa Imara na zenye Ufanisi ..... 11
1.3.3 Uwajibikaji wa Utumishi wa Umma ..... 11
1.3.4 Amani, Usalama, Utulivu na Umoja ..... 12
**Nguzo ya Kwanza** ..... 13
**Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani** ..... 13
2.1 Utangulizi ..... 13
2.2 Lengo ..... 13
2.3 Maeneo ya Yatakayozingatiwa ..... 13
2.3.1 Uchumi-jumla, Tulivu na Unaotabirika ..... 13
2.3.2 Uwiano Endelevu wa Mapato na Matumizi ..... 14
2.3.3 Ubunifu wa Vyanzo Mseto vya Fedha ..... 15
2.3.4 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji ..... 16
2.3.5 Mashirika ya Umma ya Kimkakati na yenye Ufanisi ..... 17
2.3.6 Sekta Binafsi Imara ..... 18
2.3.7 Ushirikiano wa Kimkakati wa Kikanda na Kimataifa ..... 19
Nguzo ya Pili ..... 20
Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii ..... 20
3.1 Utangulizi ..... 20
3.2 Lengo ..... 20
3.3 Maeneo Yatakayozingatiwa ..... 21
3.3.1 Jamii Iliyoelimika, yenye Ujuzi na Inayopenda Kujifunza ..... 21
3.3.2 Jamii yenye Afya ..... 22
3.3.3 Hifadhi ya Jamii Jumuishi ..... 24
3.3.4 Viwango Bora vya Maisha ..... 25
3.3.5 Nguvukazi yenye Uwezo na Motisha ..... 25
3.3.6 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Shirikishi ..... 26
Nguzo ya Tatu ..... 27
Uhifadhi wa Mazingira na Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ..... 27
4.1 Utangulizi ..... 27
4.2 Lengo ..... 27
**4.3 Maeneo Yatakayozingatiwa** ..... 28
4.3.1 Uhifadhi wa Bioanuai ..... 28
4.3.2 Uhifadhi wa Ardhioevu na Rasilimali Maji ..... 29
4.3.3 Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ..... 30
4.3.4 Usimamizi Endelevu wa Ardhi ..... 30
4.3.5 Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ..... 31
**Vichocheo vya Kufikia Malengo ya Dira** ..... 33
5.1 Utangulizi ..... 33
5.2 Lengo ..... 33
5.3 Usafirishaji fungamani ..... 33
5.4 Sayansi na Teknolojia ..... 34
5.5 Utafiti na Maendeleo ..... 35
5.6 Mageuzi ya Kidijitali ..... 36
SEKTA ZA KIMAGEUZI ..... 38

6.1 Utangulizi ... 38
6.2 Lengo ... 38
6.3 Vigezo vya Uchaguzi wa Sekta ... 39
6.4 Sekta za Kimkakati ... 39
6.4.1 Kilimo: Mazao, Mifugo, Uvuvi, na Misitu ... 39
6.4.2 Huduma kwa Watumiaji ... 40
6.4.3 Utalii ... 41
6.4.5 Uzalishaji Viwandani ... 42
6.4.6 Huduma za Fedha ... 43
6.4.8 Ujenzi na Mali isiyohamishika ... 44
6.4.9 Uchumi wa Bluu ... 46
6.4.10 Michezo na Sanaa ya Ubunifu ... 47
**UTEKELEZAJI WA DIRA** ... 48
7.1 Uwekaji wa Vipaumbele vya kimkakati ... 48
7.2 Utekelezaji wa Dira ... 48

# UTANGULIZI

Mnamo mwaka 2024, Tanzania iliadhimisha miaka 60 tangu nchi mbili huru, Tanganyika na Zanzibar zilipoungana tarehe 26 Aprili, 1964 na kuwa Jamhuri ya Muungano. Tanganyika ilipata uhuru tarehe 9 Desemba, 1961, wakati Zanzibar ilipata uhuru kamili kufuatia Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964.

Kwa zaidi ya miongo sita sasa, Tanzania imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ili kukabiliana na ujinga, maradhi na umaskini. Azimio la Arusha la mwaka 1967 liliasisi falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea likilenga kujenga usawa na mshikamano wa kijamii. Katika kipindi hicho, Tanzania ilipata mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za afya, elimu na maendeleo vijijini, sambamba na kujenga utaifa na mshikamano.

Mwaka 1985, Tanzania iliondokana na uchumi hodhi na kufuata uchumi wa soko. Mabadiliko hayo yaliweka mazingira mazuri ya ukuaji wa sekta binafsi na kupanua fursa za kiuchumi. Pamoja na mabadiliko hayo, kurejeshwa kwa mfumo wa siasa wa vyama vingi mwaka 1992, kuongeza ushiriki mpana wa kisiasa, kuliimarisha demokrasia na nafasi ya asasi za kiraia katika shughuli za utawala. Mageuzi hayo yalilenga kujenga misingi imara ya maendeleo stahimilivu.

Mnamo mwaka 2000, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ikidhamiria kufikia uchumi wa kipato cha kati kwa kupitia kilimo cha kisasa, mageuzi ya viwanda, ujenzi wa miundombinu na teknolojia. Dira hiyo imeleta mafanikio ya kuridhisha, hususan katika kuboresha hali ya maisha, ukuaji wa uchumi, utawala na kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za kisiasa na kiuchumi.

Mwaka 2020, Tanzania ilifikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya chini, ikiwa na wastani wa pato la mtu mmoja mmoja la Dola za Marekani 1,080. Hili ni ongezeko la zaidi ya asilimia 170 toka mwaka 2000. Kiwango cha hali ya maisha kiliimarika kwa kiasi kikubwa, ambapo kiwango cha umaskini uliokithiri kilipungua kutoka asilimia 36 mwaka 2000 hadi asilimia 26 mwaka 2022. Sekta za afya na elimu nazo zimeimarika zaidi: udumavu wa watoto chini ya miaka mitano ulipungua kutoka asilimia 48 mwaka 2005 hadi 30 mwaka 2022, vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi vilipungua kutoka 675 mwaka 2005 hadi 104 2022 kwa kila vizazi hai 100,000. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 112 mwaka 2005 hadi 43 mwaka 2022 kwa kila vizazi hai 1,000. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi ulifikia asilimia 100 mwaka 2020, huku kukiwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari.

**Tanzania ya Mwaka 2050**

Ifikapo mwaka 2050, Tanzania inatarajiwa kuwa taifa lenye maendeleo yanayolingana na nchi zenye uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu au zaidi. Ili kufikia hatua hiyo, kunahitajika mageuzi makubwa, ikizingatiwa ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia milioni 140, ambapo zaidi ya nusu watakuwa wanaishi mijini, na inatarajiwa wengi wao watakuwa ni vijana. Aidha, ongezeko hilo litakuwa na athari kubwa katika uhakika wa chakula, ukuaji wa miji, fursa za ajira, na upatikanaji wa huduma za elimu na afya. Hata hivyo, uwekezaji wa kimkakati katika sekta muhimu kama vile kilimo, madini, utalii, uzalishaji viwandani na teknolojia; utawezesha uchumi kukua kwa takribani mara nne ya kiwango cha sasa, hivyo, kufikia uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu cha wastani wa Dola za Marekani 4,700 mpaka 8,000 kwa mtu.

Kwa upande mwingine, wakati Tanzania ikijiandaa kuelekea mwaka 2050, italazimika kukabiliana na changamoto kadhaa zinazotokea duniani. Kuvurugika kwa mfumo unaoongozwa na kanuni za kimataifa kunaweza kuwa tishio kwa jitihada za Tanzania za kujiletea maendeleo. Vile vile, kubadilika kwa nguvu za kiuchumi na kisiasa za mataifa makubwa; kuanzishwa kwa mifumo mipya ya utangamano; na mabadiliko katika biashara za kimataifa kunaweza kuathiri utekelezaji wa Dira 2050. Changamoto nyingine duniani ni kama vile uchumi tete, kukosekana kwa usawa, ukuaji wa miji, mabadiliko ya tabianchi na ya kidemografia, mageuzi ya kiteknolojia na mivutano ya kisiasa.

Uchumi tete utaendelea kuathiri utangamano duniani, wakati pengo la usawa kati ya mataifa litaongeza tofauti za kijamii na kiuchumi. Athari za mabadiliko ya tabianchi zina madhara ya pekee kwa jamii maskini, na hivyo kulilazimu taifa kuweka vipaumbele kwenye masuala ya kukabiliana na mabadiliko hayo. Pia, mabadiliko ya kidemografia duniani yanaibua changamoto za nguvukazi kwa nchi zenye idadi kubwa ya wazee na upatikanaji wa ajira kwa nchi zenye idadi kubwa ya vijana. Aidha, maendeleo katika ukuaji wa miji na mageuzi ya teknolojia yanahitaji kuwa na ujuzi unaoendana na kasi ya mabadiliko hayo na mipango endelevu ya miji. Kutetereka kwa kisiasa za kimataifa, kunakochangiwa na dhana ya “taifa langu kwanza” na kugombea rasilimali, kutailazimu Tanzania kuimarisha diplomasia ya kimkakati.

Vile vile, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 itaendeleza mafanikio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa lengo la kuifikisha Tanzania kwenye hatua ya juu ya maendeleo. Kupitia uzoefu uliopatikana kutoka Dira 2025, na kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea duniani, Dira 2050 inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye nguvu kiuchumi barani Afrika na duniani kwa ujumla, na mustakabali endelevu, unaozingatia usawa na ustawi wa watu wake na kuwa taifa imara linaloweza kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko duniani.

## TAMKO LA DIRA

# *Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea*

Mwelekeo wa Dira 2050 ni kuwa na taifa jumuishi, lenye ustawi, haki, na linalojitegemea. Dira hii inaweka mpango madhubuti wa mageuzi ya kimaendeleo ifikapo katikati ya karne ya 21, kwa lengo la kujenga taifa linalokua, lenye usawa na linalojitosheleza. Dira najikita zaidi katika maendeleo ya watu yanayozingatia ukuaji imara wa uchumi na kukuza pato la taifa ili kuboresha hali ya maisha na kutokomeza aina zote za umaskini.

Dira 2050 imeandaliwa kwa kuzingatia historia ya mafanikio yaliyofikiwa kwa miongo iliyopita ikiwa ni pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Dira 2025, ikijumuisha mafunzo yaliyopatikana katika kutokomeza umaskini, maradhi na ujinga. Kwa kuzingatia fursa ya jiografia ya Tanzania, rasilimali zilizopo na maendeleo ya sayansi na teknolojia, Dira 2050 inalenga kupandisha ukuaji wa ato la taifa mara nne au zaidi kwa kupitia mikakati ya kimageuzi. Ukuaji huu wa kiuchumi unatarajia kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ambapo pato la mtu mmoja mmoja litaongezeka kufikia angalau Dola za Marekani 4,700.

Aidha, matarajio ya Dira 2050 ni kuwa na jamii yenye maelewano ambapo wananchi wanafurahia kuwapo kwa amani, haki na huku wakiwezeshwa kupata maarifa na ujuzi unaohitajika ili kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, pamoja na kujitosheleza kimaisha. Dira hii inasisitiza ustahimilivu na kukubali mabadiliko kama mambo muhimu katika kufikia maendeleo endelevu.

Uzingatiaji wa suala la usawa, ikiwa ni pamoja na usawa wa kijinsia, na uwezeshaji wa wanawake ni sehemu muhimu ya Dira 2050, inayoakisi misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dira hii inaweka mkazo katika ushiriki wa Tanzania kwenye itifaki za kikanda na kimataifa ili kuhakikisha taifa linabaki kuwa mwanachama hai na anayewajibika wa jumuiya ya kimataifa. Ushiriki huo unaimarisha nafasi ya Tanzania katika kuzingatia viwango vya kimataifa ili kufikia maendeleo edelevu na jumuishi. Dira 2050 inajikita katika maendeleo ya watu ambapo kila mmoja ni mshiriki na mnufaika muhimu katika maendeleo ya Tanzania.

Dira 2050 inaongozwa na misingi  sita ifuatayo:

1. **Umoja**: Kila Mtanzania ana jukumu la kudumisha Muungano, umoja na mshikamano wa kitaifa.
2. **Utu**: Kila mtu anastahili kuheshimiwa, kuthaminiwa na kulindwa utu wake.
3. **Haki za Binadamu**: Kila mtu ana haki ya kufurahia uhuru na kulindwa kwa mujibu wa Katiba.
4. **Demokrasia**: kila mtu, jamii na taifa kwa ujumla linaheshimu  na kuzingatia Katiba, mgawanyo wa mamlaka, uhuru wa mahakama, kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa,, utawala wa sheria na ushiriki sawa wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye michakato ya uamuzi.
5. **Ulinzi wa Maliasili na Rasilimali:** Maliasili na rasilimali za Tanzania ni vitu vyenye thamani kubwa kwa watu wake. Hivyo, zinapaswa kusimamiwa, kulindwa na kutumiwa vema kwa maendeleo endelevuna ustawi wa taifa, na kwa manufaa ya kizazi cha leo na vizazi vijavyo.
6. **Ulinzi wa Utamaduni na Maadili ya Taifa:** Urithi wa utamaduni wa Tanzania na maadili ya taifa vitahifadhiwa, kukuzwa na kulindwa ili kujenga utambulisho wa kitaifa na umoja, na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Dira 2050 inaweka msingi imara wa kukuza jamii yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za sasa na za baadaye. Hivyo, Dira hii inazingatia ajenda ya mabadiliko yenye lengo la kutokomeza aina zote za umaskini, kukuza mfumo wa utawala wa haki na jumuishi, kufikia ukuaji wa uchumi wenye wigo mpana, kukuza uwezo wa  kila mtu, utunzaji endelevu wa mazingira, na kulinda rasilimali za taifa kwa vizazi vijavyo.


Malengo ya Dira 2050 ni haya  yafuatayo:

1. Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu yenye uchumi mseto, stahimilivu, imara na jumuishi.
2. Kutokomeza aina zote za umasikini, hususan  kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, sambamba na kuimarisha maendeleo sawia kimkoa.
3. Ubora wa hali ya juu wa maisha na ustawi kwa wote.
4. Kujenga kikamilifu uwezo wa watu wake hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
5. Mfumo wa utawala uliojumuishi wenye uwazi ambao unahakikisha amani ya kudumu, uhuru na usalama wa watu.
6. Usimamizi thabiti na endelevu wa ikolojia na rasilimali ili kujenga ustahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi.

Dira 2050 imegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:

1. ***Msingi Mkuu***: utawala, amani, usalama na utulivu. Msingi huu ndiyo jiwe la msingi la Dira 2050 linalobeba maeneo mengine. Ndiyo kusema, kuyumba kwa eneo hili kutasababisha kuyumba na hata kusambaratika kwa maeneo mengine.
2. ***Nguzo***: kuna nguzo tatu zinazobeba Dira 2050: uchumi imara, jumuishi na shindani; uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; na uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Kufikiwa kwa lengo la Dira kunategemea ufanisi katika utekelezaji wa nguzo hizi.
3. ***Vichocheo***: ni maeneo yanayochochea kasi ya utekelezaji wa maeneo mengine ya Dira ili kuleta tija, ufanisi na ubunifu.
4. ***Sekta za Kimageuzi***: hizi ni sekta za kipaumbele ambazo utekelezaji wake unatarajiwa kuchagiza na kuwezesha ukuaji wa uchumi kufikia lengo la taifa la kuwa na uchumi wa kati ngazi ya juu.

Muhtasari wa muundo wa Dira 2050 umeoneshwa katika Kielelezo namba moja.




Kielelezo 1: Muundo wa Dira 2050

# Shabaha za Jumla za Taifa Ifikapo Mwaka 2050

1. Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati ngazi ya juu, ukichagizwa na sekta ya uzalishaji viwandani. Lengo ni kufikia pato la mtu, kati ya Dola za Marekani 4,700 na 8,000, na pato la taifa kufikia zaidi ya bilioni 700 za Dola za Marekani ifikapo mwaka 2050.
2. Kuondoa umaskini uliokithiri na kupunguza kiwango cha umaskini wa mahitaji kuwa chini ya asilimia 5.
3. Tanzania kuwa nchi kinara katika uzalishaji wa chakula barani Afrika, na kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa kumi wa chakula duniani.
4. Kuwa na mazingira bora ya kufanya biashara, na kushika nafasi ya tatu bora barani Afrika katika kuvutia wawekezaji.
5. Kuwa na sekta binafsi imara na yenye ujasiri na uwezo wa kushindani kikanda na kimataifa.
6. Kiswahili kuwa lugha inayoheshimika na kutumika kama moja ya lugha rasmi mbili katika ukanda wa Afrika na moja ya lugha rasmi zinazotumika katika Jumuiya ya Umoja wa Mataifa.
7. Kuwa na mfumo bora wa elimu katika ngazi zote unaojenga maarifa na stadi za wahitimu na wenye kushabihiana kwa karibu na sekta za uzalishaji.
8. Kuwa na jamii yenye afya njema ambapo kila mtanzania anapata huduma bora za afya, maji na makazi bora.
9. Kuwa taifa linalojitegemea katika mahitaji ya umeme ambapo wastani wa matumizi ya umeme kwa mtu yatakuwa angalau kWh 600.
10. Kuwa na jamii inayothamini uhifadhi wa mazingira na iliyo tayari kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.
11. Tanzania kuwa kitovu cha huduma za usafirishaji mizigo ya kibiashara katika ukanda wa Afrika.
12. Kuwa na jamii yenye maarifa ya kidijiti na yenye uwezo wa kutumia zana na kuzalisha teknolojia za kidigiti katika huduma na uzalishaji.
13. Tanzania kuwa taifa la kidemokrasia, likiongozwa na katiba imara inayoakisi mwafaka wa kitaifa, taasisi madhubuti za umma, na mfumo thabiti wa vyama vingi vya siasa.
14. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 bora duniani na kushika nafasi ya kwanza barani Afrika katika kupunguza pengo la kijinsia kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2050.
15. Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kwa wanaume na wanawake kufikia miaka 75.
16. Tanzania kuwa nchi kinara barani Afrika kwa vivutio vya utalii na miongoni mwa nchi tatu bora barani Afrika zinazotembelewa na watalii kwa wingi.
17. Kila Mtanzania kuwa na elimu angalau ya kidato cha nne, na angalau asilimia 15 ya Watanzania kuwa na elimu ya juu, wakiwa na ujuzi stahiki unaolingana na mahitaji ya soko la ajira na ulimwengu unaobadilika.
18. Angalau mtu mmoja katika kila watanzania wawili wenye sifa za kuajiriwa kuwa wameajiriwa katika sekta rasmi na wakiwa na mikataba kamili ya ajira.
19. Watanzania wote wanafurahia uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa kukusanyika katika mazingira ya amani, usalama na utulivu.
20. Ardhi yote ya Tanzania kupangwa na kupimwa kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na uwekezaji.

# Msingi wa Dira

## Utawala, Amani, Usalama na Utulivu

### 1.1 Utangulizi

Dira ya 2050 inajengwa katika msingi imara unaozingatia matakwa ya kikatiba, mfumo wa demokrasia, ugatuzi wa madaraka, na utamaduni wa kisiasa unaokuza ujumuishi, hivyo kuweka misingi ya utawala bora, amani, usalama na utulivu. Hii ni pamoja na kudumisha utawala wa sheria na haki, na kulinda haki za msingi na uhuru. Pia, inahusisha kuhakikisha kuwa kuna usalama na uadilifu, kukuza taasisi za kiraia zenye nguvu, kuimarisha utendaji wa utumishi wa umma, kukuza uhuru wa taasisi, usawa wa kijinsia, umoja wa kitaifa, na amani, huku ikilinda usalama na uadilifu wa taifa.

Tangu ilipopata uhuru, Tanzania imejenga umoja wa kitaifa, pamoja na mambo mengine, kupitia ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kuunganisha, kupanua ushiriki wa kisiasa, na kufanya mageuzi ya kikatiba. Hatua za makusudi zimechukuliwa kurekebisha changamoto ya kihistoria ya kukosekana kwa usawa kwa kuboresha upatikanaji wa rasilimali, usawa wa kijinsia, huduma muhimu za kijamii, na kutekeleza sera na mipango ya maendeleo jumuishi, yenye wigo mpana na inayolenga maendeleo ya watu. Aidha, Serikali imefanya mageuzi ya mfumo wa utoaji haki ili kuimarisha ufanisi na kuboresha usimamizi wa mahakama na kuimarisha mfumo wa haki jinai. Dira 2050 itaendeleza utawala bora, haki za binadamu, demokrasia, na kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, na uwajibikaji.

### 1.2 Lengo

Kuwa na mifumo imara ya kisheria na kitaasisi katika kuwezesha utekelezaji endelevu na wenye ufanisi wa Dira 2050.

### 1.3 Maeneo Yatakayozingatia

#### 1.3.1 Utawala Bora na Haki ya Jamii

Utawala bora ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi, na kuhakikisha maendeleo endelevu. Utawala bora unazingatia misingi ya kikatiba, na mfumo wa demokrasia. Vile vile, utawala bora unahusu utawala wa sheria, kulinda haki za binadamu, , kukuza taasisi imara za kiraia, uwajibikaji na weledi katika utumishi wa umma, usawa wa kijinsia, umoja wa kitaifa na amani.

**Matarajio**

a) Taifa linaloheshimu na kuzingatia demokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu, na uwajibikaji kwa wote.
b) Taifa linalopiga vita aina zote za ukatili, ikiwa ni pamoja na ukatili wa kijinsia, ukatili kwa watoto na kwa watu wenye ulemavu.
c) Taifa linalotambua, kuheshimu na kulinda uhuru wa asasi za kiraia.
d) Kuwa na uongozi imara, unaozingatia weledi, usawa wa kijinsia, na uandaaji wa kizazi cha viongozi wa baadaye ili kuhakikisha uendelevu katika kutekeleza malengo ya kitaifa.
e) Kuwa na Katiba imara yenye muafaka wa kitaifa inayoakisi muafaka endelevu wa kitaifa.

### 1.3.2 Serikali za Mtaa Imara na zenye Ufanisi

Baada ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, kulifanyika mageuzi ya utawala wa serikali za mitaa mwaka 1962 ambapo mamlaka za wenyeji zilifutwa ili kukuza umoja wa kitaifa. Aidha, mwaka 1972, Serikali ilizifuta mamlaka za serikali za mitaa. Hata hivyo, mnamo mwaka 1982, serikali za mitaa zilirejeshwa. Licha ya Tanzania kuanzisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ya utawala wa serikali za mitaa, mamlaka za serikali hizi bado zinakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na mamlaka ya kutosha katika kufanya maamuzi, usimamizi duni wa rasilimali na uwezo mdogo wa kifedha.

**Matarajio**

a) Taasisi za serikali za mitaa zilizo imara, zinazojitegemea, bunifu na zisizo na rushwa ili kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa jamii na kuhakikisha mahitaji yao yanatimizwa kwa ufanisi na usawa.
b) Mfumo ulio wazi na wenye ufanisi wa kukusanya na kugawa rasilimali fedha kati ya serikali kuu na serikali za mitaa, kuhakikisha kuwa kuna mgawo sawia kwa kuzingatia mizania ya kimkoa.
c) Mfumo wa huduma za serikali za mitaa unaozingatia sifa na weledi katika kuajiri na kupandisha madaraja.

### 1.3.3 Uwajibikaji wa Utumishi wa Umma

Wananchi wana jukumu muhimu kwenye utawala katika kutetea masilahi yao, kukuza uwazi, ujumuishi na kuiwajibisha serikali pale inapobidi.

Ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma unahakikisha kuwa sera na huduma zinazingatia mahitaji yao, viwango vya maadili, na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma, na hatimaye kuchangia kufikiwa kwa malengo yanayotarajiwa.. Ubora wa huduma za umma unachangia kwa kiasi kikubwa ufanisi katika masuala ya utawala kwa kuwezesha utekelezaji mzuri wa sera, utoaji wa huduma, na usimamizi wa masuala ya serikali. Hata hivyo, utumishi wa umma nchini Tanzania bado unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo ya upungufu wa rasilimali watu, ujuzi mdogo kwa baadhi ya watumishi na wengine kutokufanya kazi kwa weledi .

**Matarajio**

a) Utumishi wa umma wenye tija na ufanisi, unaotokana na msingi wa uadilifu.
b) Utumishi wa umma unaowajibika, unaosimamia utawala wa sheria, unaopambana na rushwa, unaodumisha nidhamu na viwango vya juu vya maadili.
c) Utumishi wa umma ambapo watumishi wanaajiriwa na kutambulika kwa kuzingatia sifa, weledi na utendaji bila kujali ukabila, ukanda, itikadi za kisiasa au sababu nyingine yoyote ya kidemografia.

### 1.3.4 Amani, Usalama, Utulivu na Umoja

Amani, Amani, usalama, utulivu na umoja wa kitaifa kwa sehemu kubwa vinategemea kuwapo kwa utulivu wa ndani, mshikamano na uhusiano wa kijamii, kiuchumi na kisiasa, ambapo haki za raia zinalindwa. Changamoto ya ukuaji wa pengo la usawa, hasa miongoni mwa vijana inatishia amani, usalama utulivu na umoja. Aidha, kuna umuhimu wa kushughulikia changamoto za kiuchumi na kijamii zinazohusiana na usalama wa watu, hasa migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, ukuaji wa tatizo la ajira kwa vijana na ukatili wa kijinsia.

Kulinda mamlaka, uhuru na usalama wa Tanzania ni muhumu katika muktadha wa sasa wa kikanda na kidunia. Kwa upande wa changamoto za nje, mitikisiko ya kikanda na ya kidunia, ikiwemo kukosekana kwa amani katika mataifa jirani na mabadiliko ya kiuchumi duniani, vinaweza kuathiri maendeleo ya nchi yetu.

**Matarajio**

a) Kuwa na Muungano imara na endelevu kama nyenzo ya kulinda umoja, amani, utangamano na ustawi kwa wote.
b) Kuwa na taifa lenye mifumo imara na miundombinu ya kisasa ya kutambua na kudhibiti vihatirishi mbalimbali vya usalama na amani dhidi ya aina zote za vita.
c) Kuwa nchi kinara wa amani katika bara la Afrika na kushiriki kikamilifu katika kuzuia migogoro, usimamizi wa amani, upatanishi ili kuimarisha utulivu na ustawi wa kimataifa.

# Nguzo ya Kwanza

## Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

### 2.1 Utangulizi

Uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara, tulivu na kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 6.4 kwa zaidi ya miongo miwili. Hata hivyo, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uchumi mkuu hayakuweza kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. Ukuaji huo ulitokana na sekta chache za uzalishaji, tija ndogo na mauzo ya nje hafifu, hivyo kuathiri ongezeko la ajira, fedha za kigeni, kasi kupunguza umaskini wa kaya. Aidha ukuaji huu wa si himilivu dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi.

Uchumi umeambatana na ukuaji wa miji ambao umechochea ongezeko la ajira za kipato cha chini na biashara isiyo rasmi . Nguvukazi na rasilimali nyingine zimehama kutoka kwenye sekta ya kilimo na kwenda kwenye sekta zenye tija ndogo, badala ya uzalishaji viwandani na sekta za huduma zenye tija kubwa. Uchumi wa aina hii umewaacha watu wengi kwenye sekta isiyo rasmi, hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Vile vile, ukuaji huu mdogo umezuia ongezeko la biashara ya nje, umeathiri ongezeko la thamani, na hivyo nchi kushindwa kutumia vizuri fursa za masoko ya kikanda na ya kimataifa.

Matarajio ya Dira ni kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2050. Ili kufikia lengo hili, inahitajika kasi ya ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 10 kwa mwaka. Aidha, uchumi huu unapaswa kuwa jumuishi na shindani, na utategemea mchango wa sekta mchanganyiko, utakaojengwa kupitia sera na mazingira wezeshi yatakayovutia uwekezaji na biashara.

### 2.2 Lengo

Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuimarisha ushindani na uwazi, na kuwezesha utabiri wa sera za kiuchumi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

### 2.3 Maeneo ya Yatakayozingatiwa

#### 2.3.1 Uchumi-jumla, Tulivu na Unaotabirika

Msingi wa uchumi imara na endelevu ni matokeo ya uchumi-jumla tulivu na unaotabirika unajengwa na uwiano mzuri wa viashiria muhimu vya uchumi kama vile

mahitaji na upatikanaji wa bidhaa na huduma, urari wa malipo, mapato na matumizi ya serikali, pamoja na akiba na uwekezaji. Mfumuko wa bei na viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni vimekuwa katika udhibiti mzuri. Aidha, kwa zaidi ya muongo mmoja mfumuko wa bei umebakia katika tarakimu moja, na thamani ya shilingi imeendelea kuwa tulivu. Mafanikio haya yametokana na sera imara za uchumi za nchi, sheria, mifumo wezeshi ya udhibiti, na kitaasisi. Pamoja na mafanikio hayo, maendeleo zaidi katika utulivu wa uchumi-jumla na wenye kutabirika vinahitajika ili kuchochea ukuaji wa uchumi na uwekezaji.

**Matarajio**

a) Mazingira tulivu ya uchumi-jumla unaoendana na mahitaji na upatikanaji wa huduma na bidhaa, urari wa malipo, mapato na matumizi ya serikali pamoja na akiba na uwekezaji.
b) Sera za fedha na kikodi zinazotabirika na zenye uwazi ili kuvutia ukuaji wa uwekezaji wa ndani na nje

### 2.3.2 Uwiano Endelevu wa Mapato na Matumizi

Uwiano wa mapato na matumizi ni hali ambayo serikali inakuwa na uwezo wa kudhibiti mapato na matumizi na deni la taifa bila kuongeza mzigo wa kifedha na deni la taifa au kuathiri ukuaji wa uchumi wa muda mrefu. Huu ni msingi wa kujenga uchumi imara na wenye ushindani. Inajumuisha mikakati ya kuboresha usimamizi wa bajeti, kupunguza nakisi ya bajeti, na kuhakikisha kuwa serikali inakidhi mahitaji yake ya kifedha kwa ajili ya ukuaji wa uchumi endelevu. Kwa kipindi cha miongo miwili iliyopita, Tanzania imefanya mageuzi mbalimbali yenye lengo la kuimarisha uwezo wake wa kifedha na kuboresha usimamizi wa matumizi. Hatua hizo ni pamoja na kupanua wigo wa kodi, kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kutumia teknolojia za kidijitali, kuboresha uwazi na elimu kwa mlipakodi, usimamizi wa matumizi na ukaguzi.

Pamoja na mafanikio haya, wigo wa kodi umebaki kuwa finyu, wenye ufanisi mdogo, na uwiano wa kodi na pato la taifa wa kiwango cha chini ukilinganishwa na nchi zenye uchumi unaolingana na Tanzania. Usimamizi wa kodi umethiriwa kwa kiwango kikubwa na mazingira ya biashara yasiyorafiki baina ya mlipa kodi na mamlaka za ukusanyaji kodi. Aidha, ongezeko la matumizi ya Serikali limesababisha kuongezeka kwa ukopaji huku mikakati ya usimamizi wa madeni ukipunguza uwezekano wa sekta binafsi kupata mikopo. Vilevile, maboresho katika usimamizi wa matumizi ya Serikali yameimarisha utoaji wa taarifa na usimamizi pasipo kuboresha mfumo wa kuweka vipaumbele vya kimakakati. Kumekuwa na mtazamo kwamba uwekezaji katika sekta ya umma una tija kuliko matumizi ya kawaida ambayo yanonekana kutokuwa na tija.

Mtazamo huu unashindwa kuzingatia kwamba matumizi ya kawaida pia yanachochea ukuaji wa uchumi, hususan katika muktadha wa ukosefu wa ajira.

Aidha, usimamizi wa deni la taifa ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa uwiano wa mapato na matumizi ya kifedha. Suala hili linahitaji uwajibikaji na uwazi, pamoja na usimamizi bora wa uwekezaji. Kwa sasa, deni la taifa linatajwa kuwa stahimilivu.

**Matarajio**

a) Mfumo wa kodi wenye usawa, ufanisi na tija, unaoboresha uwiano kati ya kodi na pato la taifa, na kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo
b) Mfumo wa kikodi wenye uwazi na unaotabirika, unaowezesha kuanzisha, kukuza na kurasimisha biashara, ili kutoa fursa za ajira, na kupanua wigo wa walipa kodi.
c) Usimamizi thabithi wa deni la taifa na kuhakikisha linakuwa himilivu na endelevu na mgawanyo bora wa rasilimali bora wa raslimali za taifa.
d) Usimamizi thabiti wa bajeti unazingatia vipaombele vya taifa na thamani ya fedha katika matumizi ya serikali.
e) Mipango ya bajeti inayohakikisha uwiano wenye tija baina ya uwekezaji kwa ajili ukuaji wa baadaye,na matumizi ya kawaida kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa sasa.

### 2.3.3 Ubunifu wa Vyanzo Mseto vya Fedha

Ugharimiaji wa maendeleo nchini Tanzania unategemea vyanzo vya mapato mbalimbali, vikiwemo kodi, ushuru na tozo, mikopo ya ndani na nje, uwekezaji wa kigeni, mikopo na misaada. Pamoja na umuhimu wa vyanzo vilivyopo sasa ni muhimu kubuni na kuibua vyanzo vipya, ajili kuimarisha uwezo wa mapato yatakayokidhi mahitaji ya maendeleo. Vyanzo vipya ni pamoja na masoko ya fedha na mitaji, ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi , uhisani wa kibinadamu, v*enture capitial* na *angel capital*. Tanzania inatekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha vyanzo anuai vya mapato, ikiwemo soko la fedha na mitaji la Dar es salaam na mifumo ya yake kama vile mamlaka ya masoko ya mitaji na dhamana. Aidha, Tanzania imeanzisha Kituo cha ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kukuza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Vile vile, Benki Kuu ya Tanzania imekua ikiboresha masoko ya kifedha nchini kwa kuweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na miundombinu bora ya soko la fedha, kuweka sheria zinazofaa na kuwezesha maendeleo ya ubunifu wa fedha na zana za soko la mitaji

Hata hivyo, kwa ujumla, kuna mapokeo duni ya dhana ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Aidha, soko la fedha ni dogo na linakwepa vihatarishi (risk-averse), wakati soko la mitaji bado liko katika hatua za awali na kukosa nguvu ya mabadiliko. Hatua

zinaendelea za kuongeza soko la fedha na mitaji ni muhimu ili kukabiliana na changamoto hizi kwa ufanisi.

**Matarajio**

a) Kuongezeka kwa matumizi thabiti ya mfumo wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kama njia ya kugharimia na kuendeleza miradi ya maendeleo.
b) Soko la fedha na mitaji lenye ubunifu, ufanisi na tija, lililojengwa juu ya misingi wezeshi ya kisheria inayozingatia uwazi, usawa, uwajibikaji na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa washiriki wote.
c) Kuwa na mifumo ya mitaji jumuishi inayolenga kuyawezesha makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
d) Jamii ya wajasiriamali imara yenye mtazamo wa uthubutu na nidhamu ya kuchukua mikopo kama njia ya kupata mitaji ya miradi ya maendeleo.
e) Mfumo thabiti wa ikolojia ya vyanzo mbadala vya fedha na mitaji kama vile mitaji binafsi.

### 2.3.4 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji

Uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote unategemea mazingira rafiki ya biashara. Tanzania imetekeleza mipango mbalimbali ya kuboresha mazingira ya biashara ikiwamo kupitia upya sheria na kanuni, kupunguza na kuondoa ada na kodi na kuoanisha majukumu ya vyombo vya udhibiti. Mipango hii inalenga kuimarisha ufanisi wa mifumo ya sheria, kurahisisha utawala na udhibiti wa biashara na kuongeza uwazi katika michakato ya udhibiti.

Pamoja na jitihada hizi, mabadiliko makubwa hayajaanza kuonekana. Changamoto nyingi zimeendelea kuwepo, zikijumuisha: gharama kubwa katika mchakato wa uwekezaji ikiwamo kodi na tozo pamoja na muda wa kuanza biashara, muda mrefu wa kukamilisha taratibu za awali za uidhinishaji wa biashara na uwekezaji, na kuongezeka kwa urasimu usiokuwa na tija. Aidha, changamoto nyingine ni: udhibiti uliokithiri hususani katika kudhibiti kodi na mapato kwa bidhaa zenye thamani kubwa; migongano ya sera, sheria, kanuni na majukumu ya taasisi za udhibiti. Aidha, wafanyabiashara wanakabiliwa na mzigo mkubwa wa kodi, ada, na ongezeko la gharama kutokana na mahitaji mengi ya leseni, vyeti na vibali, vinavyochangiwa na vyombo vya udhibiti vilivyopewa jukumu la kukusanya mapato.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, juhudi za ziada zinahitajika kuimarisha mazingira ya biashara na hivyo kukuza uchumi na uwekezaji.

**Matarajio**

a) Nchi inayoongoza kwa kuvutia uwekezaji ikiwa kati ya nchi tatu bora katika bara la Afrika kwa wepesi wa kufanya biashara na uwekezaji;
b) Sera endelevu na zinazotabirika ili kuweka mazingira bora ya uwekezaji yanayovutia makampuni ya ndani na nje;
c) Uchumi mpana unaotokana na ongezeko, ukuaji na uendeleaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati pamoja na kampuni kubwa shindani za kimataifa;
d) Mfumo jumuishi na unaobadilika na kuchangia ukuaji endelevu wa biashara na kutoa motisha ili kuzalisha ajira.na;
e) Jamii yenye utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza ili kutengeneza utajiri na kuwa na maisha bora.

### 2.3.5 Mashirika ya Umma ya Kimkakati na yenye Ufanisi

Mashirika ya umma yana mchango mkubwa kwenye uchumi, hususani, kwa sekta zenye masilahi makubwa ya taifa. Hata hivyo, mashirika mengi kwa sasa hayaendeshwi kwa ufanisi na faida, hali inayochangiwa na kukosekana kwa uhuru wa uendeshaji na fedha, na hivyo kuendelea kuwa mkondo wa kutumia fedha za umma. Aidha, mashirika haya yanashindana na kampuni binafsi kuuza bidhaa na wakati mwingine kutoa huduma katika maeneo yasiyo ya kimkakati.

Mashirika ya umma yanapaswa kuelekeza uwekazaji wake kwenye maeneo ya kimkakati yenye masilahi ya nchi kama vile nishati, usafirishaji na huduma muhimu za umma. Kwa kufanya hivyo, sekta ya umma itachangia kuweka msingi wa maendeleo mapana ya uchumi, kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuongeza ufanisi wa soko.

Ili kuyafanya haya, uendeshaji wa mashirika ya umma unapaswa kufanyika kwa uwazi na ufanisi, kuhakikisha ushirikiano badala ushindani utakaozibana sekta binafsi. Ukuzaji wa mashirika ya umma yanayosimamiwa vizuri ukiongozwa na malengo bayana ya kimkakati utawezesha ukuaji endelevu, kuzalisha ajira na kuongeza mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kuendana Dira ya 2050. Mkabala huu unaonesha umuhimu wa mchango wa mashirika ya umma kama mdau wa moja kwa moja na mwezeshi wa uchumi imara, anuwai na himilivu.

**Matarajio**

a) Kuwa na mashirika umma imara yaliyojengwa kwenye msingi wa uadilifu, uwazi, uwajibikaji na usimamizi thabiti kwa lengo la kuongeza mchango wa kijamii na kiuchumi huku yakishirikiana na sekta binafsi kukuza uchumi jumuishi na maendeleo ya taifa;

b) Mashirika ya umma yanayojiendesha yenyewe kwa faida na kuvutia uwekezaji mpana ili kuongeza kasi ya maendeleo ya uchumi na hivyo kuwezesha utoaji wa huduma kwa umma;
c) Mashirika ya umma yenye uwezo wa kushindana kitaifa na kimataifa katika soko kwa ubunifu pasipo kuathiri matumizi ya rasilimali za umma katika vipaumbele vya maendeleo.
d) Mashirika ya umma yanayoweza kumudu ushindani wa kimataifa na kuwezeshwa kimkakati kukuza viwanda, maendeleo ya miundombinu, na ukuaji wa kiuchumi huku yakizingatia ushirikiano na sekta binafsi.

### 2.3.6 Sekta Binafsi Imara

Sekta binafsi yenye nguvu na inayowajibika ni injini ya uchumi imara na endelevu. Jitihada zimefanywa kushirikisha na kukuza ushiriki wa sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na majadiliano ya sekta ya umma na binafsi na kuanzishwa kwa mfumo na sera ya ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi. Pia, diplomasia ya kiuchumi imekuwa ni kipengele muhimu katika sera ya mambo ya nje. Aidha, mipango kadhaa ya ujumuishaji wa kifedha imetekelezwa ili kuongeza upatikanaji wa mtaji wa kifedha.

Hata hivyo, sekta binafsi nchini Tanzania bado inaongozwa na kampuni ndogo na za kati, nyingi zikiwa zinafanya kazi isivyo rasmi bila rasilimali za kutosha. Sera za kisekta zinazohimiza matumizi ya rasilimali za ndani katika miradi ya maendeleo zinalenga kuzinufaisha kampuni zinazomilikiwa na Watanzania zimefanikiwa kwa kiasi kidogo kutokana na uwezo mdogo wa utekelezaji na usimamizi.

Kumekuwa na jitihada za kuandaa sera ya taifa inayohimiza matumizi ya rasilimali za ndani katika miradi ya maendeleo kama njia mbadala ya ushiriki mdogo wa kampuni za ndani katika miradi ya uchumi. Mafanikio ya sera hii yatategemea ufanisi katika utekelezaji na usimamizi.

**Matarajio**

a) Huduma ya umma inayolenga sekta binafsi ili kukuza mazingira wezeshi ambapo biashara binafsi zinaweza kustawi na kuchangia kwa ufanisi katika maendeleo ya kiuchumi.
b) Sekta binafsi yenye ushindani, imara, na jumuishi ambayo inaongoza maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
c) Sekta binafsi inayoweza kushindana katika soko la kimataifa kwa kutumia nafasi iliyo nayo katika mnyororo wa thamani kimataifa.
d) Kupungua kwa kiasi kikubwa idadi ya sekta zisizo rasmi katika uchumi.

### 2.3.7 Ushirikiano wa Kimkakati wa Kikanda na Kimataifa

Tanzania inatambulika kama kinara katika harakati za ukombozi kwa nchi za kusini mwa Afrika na katika mpango wa urejeshaji wa amani na utatuzi wa migogoro katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu. Ingawa ushiriki wa kimataifa kwa siku za karibuni umezingatia zaidi diplomasia ya uchumi, mkabala mpana shirikishi unapaswa kutiliwa maanani ili kuzingatia upekee wa Tanzania. Tanzania inaweza kupata ushawishi na ustawi wake wa muda mrefu kwa kuweka pamoja vipengele muhimu vya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

Ikiwa Tanzania itaimarisha uongozi wake ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki , Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika,na Umoja wa Afrika ; utaiwezesha kuandaaa sera za kikanda, kuimarisha biashara na uwekezaji, na kuimarisha jukumu lake katika kuleta utulivu wa kiuchumi na kisiasa. Kuiweka Tanzania kama daraja kati ya Afrika Mashariki na Kati na masoko yanayochipukia katika Bara la Asia na Amerika ya Kusini kutavutia uwekezaji, uhamishaji wa teknolojia, na kupanua fursa za biashara nje, huku kukikuza sauti ya Tanzania kuhusu masuala ya kimataifa kama biashara, maendeleo endelevu, na hali ya hewa. Aidha, kuimarisha diplomasia ya utamaduni wa Tanzania kutaipa nguvu, na kuifanya kuwa kivutio cha utalii, kubadilishana utamaduni, na elimu. Utekelezaji Madhubuti wa Mkakati wa Diplomasia ya Utamaduni utainua hadhi ya Tanzania na kuimarisha uhusiano wake kimataifa.

**Matarajio**

a) Ushirikiano na uongozi katika ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika kupitia mipango inayoendelea ya kujenga amani, upatanishi, na kuongeza ushawishi katika mifumo ya sera za usalama wa kikanda.
b) Ushirikiano thabiti wa kimkakati uliojengwa kwenye misingi ya uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia na nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi, kwa lengo la kuwezesha uwekezaji na uhamishaji wa teknolojia.
c) Uimarishaji wa masuala ya kiutamaduni, ikiwa ni pamoja na kukuza Kiswahili kama lugha ya kikanda na kimataifa na uzoefu wa kitamaduni.
d) Kiungo muhimu kimataifa, katika kutetea masilahi ya Afrika katika majukwaa ya kimataifa kuhusu masuala muhimu kama vile haki za bindamu, mabadiliko ya tabianchi, haki ya kiuchumi, na maendeleo endelevu.

# Nguzo ya Pili

# Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

### 3.1 Utangulizi

Rasilimali watu iliyoendelezwa vizuri ni msingi imara kwa Tanzania kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, msisitizo ukiwekwa kwenye malezi na makuzi ya mtu tangu utotoni hadi utu uzima. Uwezo wa binadamu ni zaidi ya uzalishaji wa kiuchumi; unajumuisha uhuru, ujuzi, na na fursa mbalimbali zinazomwezesha mtu kuishi Maisha bora. Hivyo basi, Dira ya Taifa 2050 inatoa kipaumbele katika kujenga na kuendeleza rasilimali watu na maendeleo ya mtu kwa ujumla, kwa kuzingatia malezi na makuzi bora ya mtoto kuanzia ngazi ya awali, pamoja na ujifunzaji endelevu. Hii ni hatua muhimu katika kumuandaa mtu kukabiliana na mahitaji ya kijamii na ya kiuchumi ya sasa nay a baadae.

Elimu bora na mafunzo, huduma za afya na ustawi pamoja na kinga, ulinzi wa jamii, na ushiriki wa jamii katika mambo mbalimbali ni msingi wa mkakati wa maendeleo ya watu wa Tanzania, unaoendana na malengo ya Dira ambayo ni kutokomeza umaskini, kukuza uchumi, na kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii.

Jamii yenye maarifa na ujuzi ni nguzo muhimu ya mafanikio ya kijamii, kiuchumi, na ushindani wa kimataifa. Upatikanaji wa huduma bora za kijamii huwapa wananchi uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kujenga maendeleo endelevu ya taifa. Dira ya Taifa 2050 inaweka mkazo katika elimu na mafunzo bora katika kila ngazi ya elimu, kuhakikisha jamii yenye afya bora, usawa wa kijamii, makazi bora, na kuwajengea wananchi uwajibikaji kwa maendeleo ya pamoja. Aidha, Dira hii inalenga kuzalisha nguvukazi madhubuti, yenye ujuzi wa hali ya juu, bidii ya kazi, na mshikamano ifikapo mwaka 2050.

### 3.2 Lengo

Kuwa na jamii yenye ustawi na kujenga rasimili watu yenye tija iliyo na maarifa, ujuzi, uwezo, weledi na ari inayoweza kushindana katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa.

## 3.3 Maeneo Yatakayozingatiwa

### 3.3.1 Jamii Iliyoelimika, yenye Ujuzi na Inayopenda Kujifunza

Ili kufikia ukuaji endelevu wa kijamii na kiuchumi na kushindana kwa ufanisi kimataifa ifikapo mwaka 2050, Tanzania inatarajia kujenga jamii iliyoelimika vizuri, yenye ujuzi, na inayobadilika. Dira ya 2050 inabainisha nguvu ya elimu katika kuongoza mabadiliko kwa kuwawezesha wananchi kupata maarifa muhimu, ujuzi, na maadili ili kukabiliana na changamoto za maendeleo. Elimu ni msingi wa kukuza fikra tunduizi, kutatua matatizo, ubunifu, uwezo wa uchambuzi, utaalamu katika nyanja mbalimbali, na kukuza utamaduni wa kuendelea kujifunza.

Uwekezaji katika maendeleo ya elimu ya awali ni suala lisiloepukika. Uwekezaji katika maendeleo ya watoto unaweka msingi wa ujuzi wa utambuzi kihisia na kijamii, kuandaa mazingira ya ujifunzaji endelevu na wenye mafanikio. Kwa kushughulikia mahitaji ya maendeleo, mtoto kutoka umri mdogo, hujenga nguvukazi imara, yenye ujuzi, hupunguza kukosekana kwa usawa, na kuchangia katika ukuaji wa kijamii na kiuchumi. Programu za elimu bora kwa mtoto zinasaidia katika kukabiliana na umaskini, kukuza usawa wa kijinsia, na kuwapa watoto stadi za awali za kusoma, kuhesabu, na masuala ya kijamii kwa lengo la kujenga mafanikio ya kitaaluma na kiuchumi.

Tanzania imepiga hatua katika utoaji elimu na mafunzo ikichangiwa na uwekezaji mkubwa wa serikali katika miundombinu ya shule. Mfano, kufikia mwaka 2020, kiwango cha uandikishaji wa jumla kwa elimu ya msingi kilifikia asilimia 100, na kiwango cha mpito cha msingi hadi sekondari kilifikia asilimia 73.8 mwaka 2023. Hata hivyo, mfumo huo lazima uendelee kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya jamii ya ndani na ya kimataifa ifikapo 2050.

Kuandaa vijana kwa uchumi wa dunia na mapinduzi ya viwanda kunahitaji kuweka kipaumbele katika Masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati. Ili kuziba pengo lililopo na kutatua changamoto ya uwiano wa kijinsia, hasa katika masomo yaliyobainishwa hapo juu, kunahitajika kuendeleza na kukuza uwezo wa kuhimili mabadiliko, ujasiriamali, na elimu ya masuala ya kifedha. Stadi za maisha pia ni muhimu kwa ustawi katika ulimwengu wa mabadiliko. Kupitia njia hii, mfumo wa elimu wa Tanzania unaweza kukuza nguvukazi stahimilivu, imara, itakayoweza kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Tanzania inatarajia kuona mabadiliko makubwa ya fikra, watu wenye ujasiri, na uwezo.

Dira ya Taifa 2050 inalenga kuwa nguvukazi na jamii iliyoelimika, yenye maarifa, stadi, ujuzi, maadili, fikra za kimaendeleo, na inayojiendeleza Ili kuchangia katika kuleta

maendeleo ya taifa, kukabiliana na changamoto, na kuhimili ushindani katika ngazi za kikanda na kimataifa**.**

**Matarajio**

a) Mfumo bora wa elimu na mafunzo jumuishi unaowajengea wahitimu maarifa na ujuzi, na wenye viwango vya vinavyotambulika kikanda na kimataifa.
b) Mtoto aliyepata malezi na makuzi bora, mwenye stadi msingi za maisha na ujifunzaji endelevu.
c) Wahitimu wenye ujuzi unaoendana na mahitaji ya jamii, wanaoajirika, na walio tayari kukabiliana na ushindani wa soko la ajira linalobadilika kutokana na mageuzi ya kiteknolojia.
d) Jamii iliyotumia maarifa na ujuzi, na ubunifu kama msingi wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
e) Jamii inayojifunza bila kikomo kupitia mfumo endelevu wa elimu na mafunzo, ili kujenga na kuimarisha maarifa na ujuzi wa hali ya juu kwa ajili ya kuongeza ufanisi na tija katika shughuli za kila siku za kijamii na kiuchumi kwa maendeleo endelevu.

### 3.3.2 Jamii yenye Afya

Jamii yenye afya bora ni ile ambayo mtu mmoja mmoja na jamii wanakuwa na ustawi wa kimwili, kiakili, na kijamii. Hii inajumuisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote, zenye gharama stahimilivu, uwiano sawa, mitindo bora ya maisha, na mazingira yanayosaidia kuwa na afya bora. Katika kufanikisha hili kunahitajika mfumo imara wa huduma za afya unaoungwa mkono na usaidizi mzuri wa jamii. Mfumo wa afya nchini Tanzania umepiga hatua kubwa katika miaka ya hivi karibuni, ukiweka mkazo mkubwa kwenye ujenzi wa miundombinu ili kupanua upatikanaji wa huduma katika ngazi zote nchini. Jitihada zimeelekezwa kwenye kuboresha vituo vya kutolea huduma za afya na ubora wa huduma zinazotolewa, hususan katika maeneo ya vijijini ambayo hapo awali yalikuwa hayahudumiwi vya kutosha. Mipango imeweka kipaumbele cha kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya ikiwemo dawa na vifaa muhimu, na hivyo kuimarisha uwezo wa utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote nchini. Aidha, juhudi zimeelekezwa katika ugharamiaji endelevu wa huduma afya kwa kuongeza na kutafiti uwezekano wa kutumia bima ya afya ya kijamii, kama vile bima ya afya kwa wote, ili kutoa usalama wa kifedha kwa raia. Kutokana na hayo, fahirisi ya huduma za bima ya afya kwa wote ikiwa ni shabaha kuwa na Afya kwa Wote .

Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na maendeleo makubwa katika sekta ya afya ambayo inajidhihirisha katika viashiria vya afya: Umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 51.5 mwaka 2002 hadi 66 mwaka 2022, uwiano wa vifo vya akina mama wajawazito umepungua kutoka vifo 605 mwaka 2005 hadi 104 kwa kila vizazi hai

100,000 mwaka 2022, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 67 mwaka 2016 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022.

Hata hivyo, ongezeko la kubwa la idadi ya watu (kwa asilimia 3.2 pamoja na kiwango kikubwa cha uzazi cha 4.8) na umasikini uliokithiri (asilimia 26 mwaka 2022), pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi, vinazidi kuongeza shinikizo kwenye sekta ya afya ili iweze kuboresha upatikanaji na kutoa huduma za afya bora na nafuu kwa wote. Matokeo yake, sekta ya afya inaendelea kukabiliana na changamoto kubwa, ikiwa ni pamoja na upatikanaji duni wa huduma za afya, hususan katika maeneo ya vijijini, ubora duni wa huduma za afya kwa baadhi ya maeneo, uhaba wa wafanyakazi wa afya na vifaa tiba na hitaji la ugharamiaji wa huduma za afya kwa njia endelevu ndani ya nchi.

Kuzuia na kudhibiti magonjwa ni vipaumbele vya msingi katika Sekta ya Afya ni pamoja na huduma za afya, na kuna programu zinazoendelea zinazolenga magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, ikiwemo magonjwa ya mlipuko. Juhudi hizi zinaonesha dhamira ya Tanzania ya kuboresha afya ya umma na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wote, hasa kutokana na kuongezeka kwa wasiwasi juu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, magonjwa ya moyo, magonjwa ya figo, saratani, na magonjwa ya afya ya akili.

**Matarajio**

a) Jamii iliyodhamiria kuimarisha afya na kuzuia magonjwa, wakisaidiwa na mifumo imara ya afya ya umma inayotoa kipaumbele kwa mbinu ya afya mtambuka, ufanyaji wa mazoezi, uhimilivu dhidi ya milipuko ya maradhi duniani pamoja na changamoto za afya zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.
b) Jamii yenye afya ambapo kila mwananchi anapata huduma bora za afya kwa gharama nafuu, ikiweka kipaumbele katika kuimarisha huduma za afya ya msingi na kushughulikia changamoto zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza na afya ya akili.
c) Jamii yenye afya, ambapo, wananchi wote wanalindwa dhidi ya chakula na dawa zisizofaa na ubora iwe zinazalishwa ndani au nje ya nchi
d) Jamii yenye afya ambayo hutumia teknolojia za kisasa, katika mchakato wa matibabu.
e) Bidhaa za huduma za afya zinapatikana kwa uhakika na kwa bei nafuu na zinazopatikana kwa urahisi kutoka katika viwanda vya ndani.
f) Kuwa kitovu cha huduma mahiri za ubobezi katika utoaji wa huduma za afya kwa kutumia teknolojia inayovutia tibautalii.
g) Upatikanaji wa huduma nafuu za afya kupitia mfumo mseto na endelevu wa ugharamiaji wa huduma za afya.

### 3.3.3 Hifadhi ya Jamii Jumuishi

Hifadhi ya jamii shirikishi, jumuishi, na inayozingatia usawa wa kijinsia ni muhimu katika kujenga rasilimali watu imara. Hifadhi ya jamii inaweka mifumo ya ulinzi kwa jamii na kuwajumuisha watu wote, hivyo kupunguza changamoto ya kukosekana kwa usawa.

Juhudi za hifadhi ya jamii, ushirikishwaji na usawa wa kijinsia nchini Tanzania zimeonesha mafanikio makubwa. Miradi kama vile mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania, inalenga kupunguza umaskini na kuboresha ustawi wa makundi yaliyo hatarini kama wazee na watu wenye ulemavu. Aidha, kuna juhudi za kupanua bima ya afya ili kufikia lengo la bima kwa wote.

Katika suala la usawa wa kijinsia, kumekuwa na mafanikio makubwa. Juhudi za kupunguza tofauti za kijinsia katika upatikanaji wa elimu zimefanikiwa, na kusababisha kupungua kwa pengo kwa asilimia 96, ingawa changamoto bado zipo katika vipengele vya ubora hususan katika masuala ya kijinsia. Viwango vya afya na maisha ni asilimia 97, ikiwa ni juu kidogo ya wastani wa kimataifa ambao ni asilimia 96.

Kwa kiasi kikubwa, Tanzania imeboresha upatikanaji wa huduma za maji, na usafi wa mazingira**.** Hivi sasa, asilimia 64 ya kaya zinapata angalau maji ya kunywa, na asilimia 55 ya kaya zina angalau huduma za msingi za usafi wa mazingira. Hata hivyo, upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira uko chini ya lengo la ulimwengu, na kuna tofauti kubwa kati ya maeneo ya mijini na vijijini.

Licha ya mafanikio haya, juhudi zinahitajika ili kukabiliana na changamoto zinazozuia kufikiwa kwa jamii yenye kinga jumuishi ya kijamii. Kwa ujumla, kiwango cha kinga ya jamii bado ni kidogo, ambapo chini ya asilimia 20 ya wananchi wananufaika na programu hizo, kukiwa na tofauti kubwa, kati ya jamii za mijini na vijijini, pamoja na wale walio katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Hii inaonesha hitaji la dharura la kuanzisha mipango ya hifadhi ya kijamii pana na jumuishi zaidi. Aidha, ukatili wa kijinsia bado umeenea, na tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa asilimia 44 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamepitia ukatili wa kimapenzi kutoka kwa wenza wao.

**Matarajio**

a) Jamii jumuishi isiyo na ukatili wa watoto na kijinsia ambapo kila mmoja ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu ana furaha, yuko salama, anaheshimiwa, na kuwezeshwa, kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata fursa ya kustawi.
b) Jamii inayothamini na kuhakikisha upatikanaji sawa wa fursa za kijamii na kiuchumi na uwakilishi katika majukumu ya uongozi hususani kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

c) Jamii inayofaidika na mfumo wa ulinzi wa jamii unaohakikisha kwamba kila mmoja ana uhakika wa kupata ulinzi na huduma za kijamii.

### 3.3.4 Viwango Bora vya Maisha

Viwango vya maisha vinajumuisha masuala mbalimbali ambayo huchangia kwa njia ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja tija ya mtu mmoja mmoja. Kwa kuboresha viwango vya maisha, jamii zinaweza kuongeza tija kwa jumla na kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo.

Wakati Tanzania ikiendelea kupiga hatua katika kuboresha hali ya maisha kwa watu wake, ni muhimu kuwekeza katika miundombinu na huduma muhimu ili kukuza nguvu kazi yenye tija zaidi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwapo na kupatikana kwa nyumba na makazi bora nchini kote. Pia, ni muhimu kuendeleza nyumba za gharama nafuu, kuboresha uunganishaji wa nishati ya kuaminika na ya gharama nafuu, usambazaji wa maji safi na usafi wa mazingira pamoja na miundombinu ya mawasiliano. Jitihada hizi ni muhimu katika kuimarisha viwango vya maisha, kukuza uchumi, na maendeleo ya jamii kwa ujumla nchini Tanzania.

**Matarajio**

a) Makazi bora ya gharama nafuu kwa watu wote ili kufikia maendeleo endelevu ya mijini na vijijini.
b) Upatikanaji endelevu wa maji safi na salama kwa wote, kwa gharama nafuu, na kuweka mifumo ya usafi wa mazingira, ili kuimarisha afya ya umma.
c) Mtandao himilivu wa miundombinu ya nishati kuelekea vyanzo vya nishati safi na mbadala, kukuza uendelevu wa mazingira, kupunguza uzalishaji wa kaboni, na kuimarisha usalama wa nishati katika sekta zote za jamii.

### 3.3.5 Nguvukazi yenye Uwezo na Motisha

Tanzania inaendelea kuwekeza katika kuendeleza rasilimali watu kwa kuboresha lishe, huduma za afya, ubora wa elimu, maendeleo ya ujuzi, na fursa za ajira kwa watu wake. Jitihada hizi zimewezesha kuongezeka kwa Fahirisi ya Maendeleo ya Watu - HDI kutoka 0.371 mwaka 1990 na kufikia 0.549 mwaka 2021 na nchi kupanda hadhi ya kipato kutoka kipato cha chini na kufikia kipato cha kati ngazi ya chini mwaka 2020. Kumekuwa na mafanikio makubwa ingawa kwa hatua katika kiwango cha Fahirisi ya Maendeleo ya Watu - HDI katika sekta ya afya, elimu na kiwango cha maisha. Hata hivyo, Tanzania inapaswa kuongeza juhudi maradufu katika eneo uendelezaji wa rasilimali watu ili kukuza kiwango cha Fahirisi ya Maendeleo ya Watu ambacho kipo chini wastani wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambacho ni 0.4

**Matarajio**

a) Kiwango cha uzazi ambacho kitahakikisha wastani wa idadi ya watu unaoendana uchumi na kuhakikisha maisha bora kwa wote.
b) Nguvu kazi yenye uwezo, ujuzi muhimu na utaalamu wa kukabiliana na mahitaji yanayobadilika ya masoko ya ndani na kimataifa.
c) Mazingira yanayovutia diaspora, kukuza vipaji kwa raia na wageni kwa lengo la kuimarisha rasilimali watu na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.
d) Jamii inayosisitiza uwazi, na ushindani katika soko la ajira ili kuongeza tija na ubora wa nguvu kazi.
e) Nguvukazi yenye ari na tija, itakayosaidiwa na sera imara za kazi, motisha mahali pa kazi, na jitihada za ustawi wa jamii, zisizo na ubaguzi zitakazokidhi mahitaji, ubunifu, na maendeleo endelevu.

### 3.3.6 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Shirikishi

Dira ya 2050 inalenga kujenga jamii yenye mshikamano, inayowajibika, na shirikishi inayotokana na jamii kutoka katika tamaduni mbalimbali zikiunganishwa na lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa na idadi kubwa ya vijana wenye umri wa chini ya miaka 35 ambao ni takribani asilimia 75, Tanzania inatambua uwezo wa kukuza mtaji-watu kwa kuwekeza katika mipango ya elimu, utamaduni, na michezo utakaowezesha kuimarisha mshikamano katika jamii. Nchi imeshuhudia ukuaji wa kuridhisha wa shughuli za michezo zenye ushindani, ambapo kumekuwa na uwekezaji mkubwa katika sekta binafsi. Aidha, sanaa ya ubunifu imepata mvuto, jambo litakalosaidia vipaji vya ndani kupiga hatua katika mashindano ya kikanda na kimataifa. Tanzania inataka kutumia rasilimali hizi za kitamaduni na michezo kwa maendeleo endelevu, kukuza ustawi, na kuchangia ukuaji wa uchumi.

**Matarajio**

a) Kituo mahiri cha ukuzaji wa lugha na utamaduni wa Waswahili kitakachojihusisha na utafiti na ubadilishanaji maarifa katika masuala ya kiutamaduni.
b) Watoto na vijana waliowezeshwa kwa kukuza na kuendeleza vipaji vyao ili kufikia uwezo wao kamili katika sanaa, taaluma ya michezo na burudani ndani na nje ya nchi.
c) Jamii ambayo inazingatia fikra za kimaendeleo, na kutambua muda na rasilimali kama vitu vyenye ukomo na thamani vinavyopaswa kutumiwa kwa umakini na ufanisi kwa ukuaji wa mtu mmoja na jamii.
d) Raia wanaowajibika na kujishughulisha kikamilifu katika shughuli za kijamii, wakitatua changamoto za kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa lengo la kujenga mustakabali endelevu kwa wote.
e) Raia wanaojitolea kusimamia tunu za kitaifa na kuchangia katika maendeleo ya jamii, kukuza fikra za uzalendo, uwajibikaji na kuwa sehemu ya malengo ya maendeleo ya taifa.

# Nguzo ya Tatu

## Uhifadhi wa Mazingira na Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

### 4.1 Utangulizi

Tanzania inajulikana kwa utajiri wa rasilimali za maliasili, zinazotokana na mifumo mbalimbali ya ikolojia, kuanzia uoto wa savana hadi misitu ya mvua, milima, mabonde, mito na bahari. Hii inaiweka Tanzania kuwa na maeneo muhimu zaidi ya bioanuwai duniani. Rasilimali za maliasili zinachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa taifa, ambapo utalii unaotokana na rasilimali hizi, hususani wanyamapori, misitu, na malikale, huchangia takribani asilimia 17 ya pato la taifa na asilimia 25 ya mapato yatokanayo na fedha za kigeni. Aidha, rasilimali za misitu ni muhimu sana katika uchumi wa Tanzania, zikichangia asilimia 2.5 ya Pato la Taifa na asilimia 5.9 ya biashara za nje.

Uoto wa asili, hasa misitu, umeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi hewa ukaa. Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha uzalishaji wa kaboni kwa mtu nchini ni takribani tani 0.2 kwa mwaka. Pamoja na viwango vya juu vya ukataji miti, eneo la misitu la Tanzania lina uwezo wa kuhifadhi kaboni kwa takribani gigatoni 0.4 kila mwaka. Hii inaashiria kwamba misitu ya Tanzania huhifadhi takribani asilimia 2 ya kaboni yote duniani na asilimia 11 ya kaboni inayohifadhiwa na misitu barani Afrika.

Aidha, sehemu ya uchumi wa Tanzania unategemea sekta ambazo zinaweza kuathirika na mabadiliko ya tabia nchi, sekat hizi ni pamoja na kilimo, mifugo, utalii, na uzalishaji wa umeme. Hivyo, kuongezeka kwa matukio makubwa ya athari za hali ya hewa ni hatari kwa uchumi, na kunaweza kuhatarisha usalama wa chakula, miundombinu, ajira, na afya ya umma. Kwa hiyo, Tanzania inalenga kujenga jamii yenye uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kuanzisha mfumo mzuri wa kuainisha vihatarishi vya maafa, na kuimarisha mfumo wa kuhifadhi mazingira nchini.

### 4.2 Lengo

Kufikia maendeleo endelevu yanayozingatia uhifadhi wa mazingira, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa, na kujenga uwezo wa kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### 4.3 Maeneo Yatakayozingatiwa

### 4.3.1 Uhifadhi wa Bioanuai

Mfumo wa uhifadhi wa bioanuai katika ikolojia mbalimbali nchini unahusisha ulinzi endelevu wa viumbe hai na mimea ikiwa ni pamoja na uoto wa asili wa savana, misitu ya mvua, mikoko na viumbe wa baharini, na wanyamapori. Uhifadhi huu hufanyika katika hifadhi za taifa, mapori ya akiba, maeneo ya uhifadhi wa wanyamapori wa wananchi ambayo yametengwa maalum  kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori na uwindaji uliodhibitiwa; hifadhi za misitu zinazolenga kuhifadhi mazingira ya misitu; hifadhi za bahari zilizolenga kuhifadhi maisha ya baharini. Kwa pamoja maeneo haya yaliyohifadhiwa yana ukubwa wa takribani asilimia 32 ya ardhi ya nchi, ambayo ni muhimu kwa uhifadhi wa bioanuwai, utenganishaji wa kaboni, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, na uhifadhi wa rutuba ya udongo-vitu muhimu kwa maisha ya binadamu na ustawi wa kitaifa. Bioanuai hii imeiwezesha nchi yetu kushika nafasi ya 10 kimataifa kwa uwingi wa viumbe vinavyohifadhiwa inayotambuliwa na shirika la kimataifa linalosimamia viumbe waliohatarini kutoweka duniani.

Hata hivyo, viumbe hai hawa wanakabiliwa na vitisho vikubwa kutokana na shughuli za binadamu kama vile ujangili, ukataji haramu wa miti, uvamizi wa kilimo, na upanuzi wa miji. Biashara haramu ya wanyamapori, hasa ya pembe za ndovu na nyama ya pori, inazidisha shinikizo, na kusababisha upotezaji wa bioanuwai.Katika kukabiliana na hatari tajwa, Tanzania inatekeleza sera mbalimbali zinazolenga kuimarisha kwa uhifadhi wa mazingira na viumbe hai ikiwemo Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004), Sera ya Wanyamapori Tanzania (2007), Sera ya Taifa ya Misitu (1998), na Sera ya Ufugaji Nyuki (2007), pamoja na sheria zake. Mifumo hii inasisitiza mipango ya ushiriki wa jamii za wenyeji katika uhifadhi wa bioanuwai na shughuli za kiuchumi. Aidha, ushirikiano wa kimataifa na uzingatiaji wa makubaliano ya kimataifa ya uhifadhi wa bioanuwai yanaonesha dhamira ya Tanzania katika kulinda urithi wake asilia na kuchangia katika juhudi za uhifadhi Duniani. Katika siku zijazo, juhudi endelevu ni muhimu kupunguza athari, kuimarisha hatua za uhifadhi, na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa bioanuwai kwa vizazi vijavyo.

**Matarajio**

a) Kinara duniani katika kuhifadhi wa bioanuai katika mazingira  ya asili.
b) Mfumo madhubuti ya ulinzi wa wanyamapori na mimea dhidi ya ujangili, uvunaji haramu wa magogo, uvamizi wa viumbe, na kuhakikisha uendelevu kwa vizazi vijavyo.
c) Taifa la kinara katika matumizi endelevu ya bioanuai, kwa manufaa ya uchumi wa nchi na maendeleo ya jamii.

d) Kutambua thamani halisi ya bioanuwai ili kukokotoa mchango wake katika Pato la Taifa na ukuaji wa kiuchumi na kijamii.

### 4.3.2 Uhifadhi wa Ardhioevu na Rasilimali Maji

Tanzania ina takribani hekta milioni 2.7 za eneo lenye mito ya kudumu na ya msimu, ambayo sehemu kubwa ni mabonde ya mito mikubwa barani Afrika, ikiwemo Nile, Congo, na Zambezi, pamoja na maziwa kadhaa muhimu ya kimataifa. Bonde la Rufiji linaongoza kwa kuwa na sehemu kubwa zaidi ya rasilimali za maji nchini Tanzania. Mamilioni ya watu, hasa wananchi wa kawaida, hutegemea ardhioevu kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi, hususan kilimo, nishati, na utalii. Mathalani, asilimia 37 hadi 45 ya matumizi jumuishi ya nishati hutokana na nishati ya maji.

Hata hivyo, ardhioevu hizi muhimu na vyanzo vya maji vinakabiliwa na shinikizo kubwa kutokana na uvamizi na shughuli zisizo endelevu za binadamu. Hivyo, ardhioevu inapungua kutokana na kuongezeka kwa maeneo ya kilimo na makazi, kunakosababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi ya kilimo. Kwa mfano, kukauka kwa ardhioevu kama vile ardhioevu ya Ihefu kuna madhara makubwa ya ikolojia na kuathiri siyo tu eneo la ardhioevu ya Usangu na mto Ruaha, bali pia hifadhi ya taifa ya Ruaha na ikolojia ya chini ya mto katika bonde la Rufiji, ambapo mitambo muhimu ya kufua umeme wa maji katika mabwawa ya Mtera, Kidatu, na Julius Nyerere inapatikana.

Aidha, tangu mwaka 2010, maziwa makubwa ya Tanzania yameshuhudia mabadiliko makubwa katika viwango vya maji. Mabadiliko haya kimsingi yanahusishwa na kuongezeka kwa udongo mwingi unaotokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu katika maeneo ya karibu na maziwa haya na mabadiliko ya tabianchi. Matumizi ya maji kwa mwaka nchini Tanzania ni mita za ujazo 2,300 kwa kila mtu, ambayo ni juu kidogo ya kiwango cha mita za ujazo 1,700 kwa kila mtu. Hivyo, Tanzania inachukuliwa kuwa ni nchi yenye matumizi makubwa ya maji.

**Matarajio**

a) Ardhioevu zenye ubora, thamani na kutoa huduma mbalimbali, kama vile maji safi, chakula, bioanuwai na miundombinu, ambayo inaendeleza maisha na kukuza uchumi.
b) Usimamizi endelevu wa rasilimali maji ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji pamoja na kukidhi mahitaji ya kijamii na kiikolojia kwa muda mrefu.

### 4.3.3 Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira

Uchafuzi wa mazingira nchini kwa kiasi kikubwa unatokana na ongezeko la shughuli mbalimbali za binadamu zinazosababishwa na kutokuwa na mifumo imara ya kudhibiti uzalishaji wa taka ngumu, uchafuzi wa hewa, uzalishaji wa majitaka na kelele. Kwa mujibu wa makadirio ya hivi karibuni, ongezeko la idadi ya watu wa mijini nchini ni takribani asilimia 36 ya watu wote. Kadiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanavyoongezeka, ndivyo uzalishaji wa taka ngumu na takamaji zinaongezeka, hususan katika miji mikubwa na majiji ambayo mara nyingi zinaachwa bila kushughulikiwa hivyo kusababisha hatari kubwa ya afya kwa wale wanaoishi mijini. Hivyo, uwekezaji mkubwa katika miundombinu, nyumba bora, na huduma za kudhibiti uzalishaji wa ainazote za uchafuzi wa mazingira ili kukidhi ongezeko la watu na ukuaji wa miji.

## Matarajio

a) Kuwa na jamii yenye uelewa kuhusu athari za uchafuzi wa mazingira ili kuwa na mazingira salama kwa wote.
b) Kuwa miji bora iliyojengwa kwa miundombinu ya uthibiti wa uchafuzi wa mazingira, na usimamizi uzalishaji wa taka.
c) Kuhimiza teknolojia rahisi ya matumizi ya taka kwa manufaa ya kiuchumi

### 4.3.4 Usimamizi Endelevu wa Ardhi

Tanzania ina takribani kilomita za mraba milioni moja za rasilimali ya ardhi, ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya Watanzania. Hata hivyo, kasi ya ongezeko la watu, ukuaji wa miji, upanuzi wa kilimo, uchimbaji madini, na maendeleo ya viwanda vinaongeza uhitaji mkubwa kwenye rasilimali za ardhi. Mfumo wa kisheria uliopo pamoja na mila na desturi vimechangia kukosekana kwa usawa wa kijinsia, ambao kwa kiasi kikubwa unawaathiri wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika umiliki na upatikanaji wa ardhi. Masuala mbalimbali kama vile ukosefu wa nyaraka za umiliki wa ardhi, kutokuwa na mipango toshelevu ya matumizi ya ardhi, migogoro ya mipaka ya vijiji, makazi yasiyo rasmi, uhaba wa nyumba, na ongezeko la migogoro ya matumizi ya ardhi vinasababisha ugumu katika usimamizi bora wa ardhi. Changamoto nyingine zinazochangia usimamizi hafifu wa ardhi ni pamoja na uhaba wa fedha na rasilimali watu, changamoto za kiteknolojia, na kukosekana kwa mfumo imara wa uratibu.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, Tanzania imetekeleza sera za kuimarisha usimamizi wa ardhi, ikiwamo kuimarisha usalama wa umiliki wa ardhi, kuendeleza matumizi endelevu ya ardhi, na kushirikisha jamii katika usimamizi wa maliasili. Ushirikiano wa kimataifa na msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo ni muhimu katika kuendeleza matumizi endelevu ya ardhi nchini kote. Katika siku zijazo, juhudi zinazoendelea ni muhimu katika kufikia malengo ya uhifadhi na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika muktadha wa biashara ya hewa ukaa, pamoja na maendeleo ya kiuchumi na

kijamii, kuhakikisha kwamba rasilimali za ardhi zinaweza kusaidia vizazi vya sasa na vijavyo.

**Matarajio**

a) Kuwa na taifa ambalo kila mtanzania ana haki ya kumiliki, kutumia raslimali ardhi kwa utulivu na amani.
b) Kujenga mifumo imara ya upimaji na matumizi bora ya ardhi yanawezesha na kuvutia uwekezaji wa ardhi.
c) Soko thabiti na la uwazi la biashara ya majengo ambalo linalinda masilahi ya wadau wote kupitia sekta ya ardhi inayoratibiwa vema.
d) Uwiano wa miji na vijiji kwa kuhamasisha maboresho ya kisasa na endelevu ya vijiji na miji ili kuhakikisha maendeleo jumuishi na kupunguza tofauti baina ya eneo moja na jingine.
e) Majiji na miji ya kijani, safi na endelevu, kwa ustawi, afya na maisha bora kwa wote.
f) Mfumo rafiki unaoimarisha mipaka katika maeneo ya kiutawala na ya uhifadhi ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora na yenye tija na ufanisi ya ardhi miongoni kwa watumiaji.
g) Mipaka ya kimataifa iliyopimwa na kusimamiwa.

### 4.3.5 Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, kama inavyojidhihirisha kupitia ongezeko la viwango vya joto na mvua. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, nchi hii imeshuhudia ongezeko la joto la angalau nyuzi joto 0.6 ikilinganishwa na kipindi cha miaka 1981-2010, huku maeneo mengi ya nchi yakishuhudia ongezeko la nyuzi joto 1.0 tangu miaka ya 1960. Viwango vya joto vya nchi kavu na bahari vimekuwa vikiongezeka tangu mwaka 1980, na makadirio yanaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2041, maeneo ya magharibi na maeneo ya kati yanaweza kushuhudia ongezeko la joto la zaidi ya nyuzi joto 2, huku maeneo ya mashariki yakitarajiwa kuongezeka kwa nyuzi joto moja ($1^0$).

Pamoja na kuongezeka kwa joto, kuanzia miaka ya 1970, Tanzania imekuwa ikishuhudia mabadiliko makubwa ya tabianchi yanayosababisha mvua nyingi kupita kiasi. Uchunguzi unaonesha kuwa baadhi ya maeneo ya nchi yanaweza kupata ongezeko la wastani wa mvua ya kila mwaka, hususan katika bonde la Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki, ambako inatarajiwa kutokea ongezeko kubwa la mvua za mwaka kuliko wastani. Kwa upande mwingine, maeneo ya mikoa ya nyanda za juu kusini magharibi na ukanda wa magharibi yanaweza kushuhudia ongezeko la mvua la hadi asilimia 9.9 ifikapo mwaka 2050. Mabadiliko haya yanadhihirisha changamoto kubwa kwa rasilimali za taifa, kilimo, na uhimilivu wa mabadiliko ya hali ya

hewa kwa ujumla katika nchi yetu. Mabadiliko haya pia husababisha ukame katika maeneo mengine na kusababisha upungufu wa maji, kuenea kwa magonjwa yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa, mafuriko, na kuenea kwa moto misituni pamoja na vijidudu vamizi. Pia, huchangia kupotea kwa miamba ya matumbawe na bioanuai.

Katika mazingira ya changamoto hizo, serikali imetekeleza mipango mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uandaaji wa sera na mifumo ya taasisi, pamoja na utekelezaji wake. Hata hivyo, kukosekana kwa ujumuishwaji wa kutosha wa maelekezo ya sera katika taasisi zinazotekeleza kunasababisha ukosefu wa uratibu wa kutosha. Wanawake na watoto wamekuwa waathirika wakubwa wa athari za mabadiliko ya tabianchi. Upungufu huu unaonesha hitaji la haraka la mikakati ya kina ya kupunguza na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kulinda mifumo ya ikolojia na jamii za watu.

**Matarajio**

a) Kuwa nchi kinara katika matumizi ya nishati safi, nishati mbadala na kuunda mifumo imara ya biashara ya hwa ukaa ili kupunguza uzalishaji wa gesi chafu
b) Taifa lenye mifumo ya kutoa tahadhari na uwezo wa kukabiliana, kudhibiti, kujikwamua na kupunguza athari za zitokanazo majanga ya asili na ya kibinadamu hususani mabadiliko ya tabianchi.
c) Jamii yenye ueledi, inayotumia mbinu bora na za kisasa za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.
d) Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi unaojumuisha ngazi zote za Serikali na jamii.
e) Taifa linalozingatia usimamizi thabiti wa mikataba ya kimataifa kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi.
f) Taifa linalotumia kikamilifu fursa ya biashara ya hewa ukaa ili kunufaika na fursa za fedha zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

# Vichocheo vya Kufikia Malengo ya Dira

## 5.1 Utangulizi

Dira ya 2050 inachagizwa na vichocheo vinne: usafirishaji fungamani, sayansi na teknolojia, utafiti na maendeleo, na mabadiliko ya kidijitali. Usafirishaji fungamani unarahisisha minyororo ya usafirishaji, kuboresha mgawanyo wa rasilimali na kuongeza ufanisi. Sayansi na teknolojia zinakuza uvumbuzi, zinachochea maendeleo yanayoongeza uzalishaji na ushindani. Utafiti na maendeleo ni muhimu kwa kuongeza elimu, kuibua maarifa mapya na ufumbuzi kwa ajili ya kutatua changamoto zinazoliikabili taifa na kuongeza ukuaji wa kijamii na kiuchumi. Mageuzi ya kidijitali yanawezesha kutumika kwa teknolojia za kisasa kuboresha utoaji wa huduma na ufanisi wa uendeshaji. Kwa pamoja vichocheo hivi ni muhimu sana katika kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii, kuongeza tija na ubora wa maisha kwa wananchi wote, na hivyo kufikia malengo ya Dira ya 2050.

## 5.2 Lengo

Kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia, ubunifu, na mitandao ya miundombinu ili kuongeza tija na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

## 5.3 Usafirishaji fungamani

Usafirishaji fungamani unahusisha kuoanisha mifumo ya uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi, usambazaji, na utoaji wa huduma, kwa lengo la kuongeza ufanisi.  Hivyo ni muhimu kuimarisha mifumo ya usafiri na kuwa fungamanishi ili kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika sekta ya usafirishaji kupitia uendelezaji wa kimkakati wa miundombinu, mageuzi ya kimuundo, na matumizi yateknolojia, ikitumia fursa  ya kijiografia ya kuwa lango la biashara mashariki na kusini mwa Afrika. Uwekezaji mkubwa wa mtandao wa Barabara, miundombinu ya reli hususan reli ya kisasa , upanuzi wa bandari na viwanja vya ndege, pamoja na kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania.  Vilevile, ongezeko la uzalishaji wa umeme, hasa Kituo cha Umeme wa Maji cha Julius Nyerere chenye uwezo wa megawati 2,115, vinachochea maendeleo haya. Maboresho haya yameimarisha miundombinu ndani na nje ya mipaka, hivyo, kurahisisha biashara ya kikanda na ujumuishaji wa kiuchumi. Aidha, kuanzishwa kwa Vituo vya Huduma za Pamoja Mipakani kuharakisha biashara za mipakani na matumizi ya teknolojia za kidijitali vimeboresha mchakato wa uidhinishaji wa nyaraka, usimamizi wa hesabu, ufuatiliaji wa mizigo, na ufanisi katikamifumo ya

uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi na usambazaji.. Maendeleo haya ya pamoja yanaiweka Tanzania kuwa kitovu muhimu cha usafirishaji katika kanda, kukuza ukuaji endelevu wa uchumi na kuimarisha ushindani

Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto za gharama kubwa za uendeshaji pamoja na ucheleweshwaji wa utoaji huduma. Aidha, kuna changamoto kadhaa za kisheria ikiwemo udhibiti kupita kiasi, sheria ndogo za serikali za mitaa zisizo na uwiano, na utitiri wa tozo. Kutatua changamoto hizi, juhudi zaidi zinahitajika ili kuboresha kasi ya usafirishaji na kuongeza mchango katika ukuaji wa uchumi na uzalishaji wa ajira, sambamba na kuifanya Tanzania kuwa mshindani thabiti wa kikanda na kiulimwengu.

**Matarajio**

a) Kuwa lango kuu la biashara mashariki na kusini mwa Afrika, kutumia ipasavyo fursa za kijiografia.
b) Mtandao wa usafiri fungamani wenye mfumo mseto wa usafiri ambao ni shindani, unao oanisha shoroba za kiuchumi zinazowezesha biashara za ndani na za kimataifa.
c) Watoa huduma za usafirishaji wenye viwango na wanaotumia teknolojia za kisasa za kidijitali.
d) Mazingira ya kisheria yaliyo wazi na yenye ufanisi, yanayorahisisha utozaji wa kodi, kupunguza urasimu na vikwazo, yanayoendana na maendeleo ya sekta ya usafirishaji kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

## 5.4 Sayansi na Teknolojia

Uchumi wa dunia unaobadilika kwa haraka na kuongozwa na maarifa, sayansi na teknolojia ni miongoni mwa vichocheo muhimu vya uzalishaji wenye tija, ufanisi, na ukuaji wa uchumi. Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye maendeleo ya kiteknolojia katika sekta mbalimbali. Lengo la hatua hizo ni kuongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma, uzalishaji, na hivyo, kuongeza kasi ya kuyafikia maeneo mengi hususani vijijini, hasa kupitia uwekezaji katika teknolojia za nishati mbadala kama nishati ya jua na biogasi. Aidha, matumizi ya bioteknolojia yamechangia kuongeza uzalishaji na kuimarisha ubora wa maisha katika sekta za kilimo, afya, na uzalishaji viwandani.

Serikali imechukua hatua madhubuti za kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ili kukidhi mahitaji ya jamii. Hatua hizi ni pamoja uwekezaji katika elimu, na kuhimiza masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati. Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na miundombinu duni, ukosefu wa rasilimali fedha, ujuzi duni, ushirikiano hafifu kati ya wadau, na masuala

yanayohusiana na mifumo ya udhibiti. Aidha, kukosekana kwa fursa sawa za kijinsia katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kunakwamisha ushiriki sawa baina ya wanawake na wanaume. Hali hii inachangiwa pia na ugumu katika utambuzi na uendelezaji wa vipaji.

Ili kukabiliana na vikwazo hivi, Tanzania inahitaji kupanua matumizi ya teknolojia za kisasa zinazochochea mabadiliko, ili kupiga hatua katika ajenda ya maendeleo. Mipango inayolenga kuongeza uzalishaji wa nishati mbadala itawezesha upatikanji endelevu wa nishati, wakati maendeleo katika matumizi ya bioteknolojia yanaweza kuongeza tija katika kilimo na ubunifu katika huduma za afya. Juhudi za kuongeza majukwaa ya elimu ya dijitali na tibamtandao utaziba pengo lililopo katika elimu na huduma za afya, hasa katika maeneo ya mbali.

Tanzania inatarajiwa kuwa taifa lenye uwezo wa kiteknolojia, himilivu, na jumuishi kutokana na mageuzi ya kiteknolojia ambayo yatachochea ukuaji endelevu; kuimarisha maendeleo ya watu; kukuza utawala bora; na kufungua njia ya mafanikio na usawa.

**Matarajio**

a) Kuenea kwa teknolojia zinazoibukia katika ngazi zote za uzalishaji na utoaji wa huduma ili kuongeza ufanisi na kuchochea mabadiliko.
b) Kanda za kiteknolojia zenye ubora wa kimataifa zilizojikita kwenye utafiti na ubunifu katika sekta za kipaumbele kama vile kilimo, uzalishaji viwandani na afya zikijumuisha wataalamu mahiri na rasilimalifedha ili kukidhi mahitaji ya taifa.
c) Uwekezaji madhubuti katika kuendeleza na kutumia teknolojia zinazoibukia ikiwa ni pamoja na akili unde, nishati, bioteknolojia na anga ili kusaidia ukuaji wa sekta na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

## 5.5 Utafiti na Maendeleo

Kadri nchi inavyopiga hatua katika maendeleo yake, utafiti na maendeleo ni muhimu katika kuibua ubunifu, kushughulikia changamoto za kijamii, na kuongeza tija katika sekta mbalimbali ambayo itasaidia katika kuimarisha utendaji kazi, kuboresha sera na kuinua uchumi kimataifa.

Kwa kutambua umuhimu huu, Serikali imechukua hatua kusaidia utafiti na maendeleo, ikiwa ni pamoja na kuongeza fedha za utafiti, ushirikiano na watafiti na wadau na kubidhaisha teknolojia bunifu. Hatua hizi zimechochea ongezeko la shughuli za ubunifu mathalani kuongezeka kwa kampuni changa, vituo vya ubunifu na vituo atamizi. Aidha, katika taasisi za elimu ya juu na zile zinazojishughulisha na utafiti kumekuwa na msisitizo wa kuwekeza zaidi katika utafiti na maendeleo ikiwa ni sambamba kuimarisha

miongozo inayotoa ulinzi wa kazi za kiubunifu ili kuhakikisha kwamba wabunifu wananufaika kutokana ubidhaishaji wa teknolojia zao na hivyo kukuza utamaduni wa uvumbuzi na ubunifu.

Licha ya mafanikio haya, bado kuna changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha, miundombinu duni, ujuzi mdogo, na ushirikiano hafifu kati ya wadau, jambo linalokwamisha ubunifu. Aidha, vikwazo vya kisheria, kupungua kwa wataalamu kutokana na motisha kutoka nchi nyingine inayosababisha kuchukuliwa wataalamu, uelewa mdogo wa umma, na tofauti za kijinsia vinakwamisha maendeleo na uendelevu wa mipango ya utafiti.

**Matarajio**

a) Mfumo imara wa utafiti na maendeleo unaovutia ushirikiano na asasi mbalimbali ulimwenguni ukiweka msisitizo katika ulinzi wa haki za wabunifu kwa lengo la kukuza ubunifu na uwekezaji
b) Mfumo endelevu wa ugharimiaji wa utafiti na maendeleo ambao unatenga angalau asilimia moja ya Pato la Taifa, ili kutoa motisha ya uwekezaji kwa sekta binafsi katika maeneo muhimu kama vile kilimo, bioteknolojia, nishati safi, na teknolojia zinazoibukia katika TEHAMA na nyanja zingine.
c) Taifa linafanya uamuzi kwa kutumia matokeo ya ushahidi wa kisayansi kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi
d) Kitovu cha ubunifu wa kikanda kinachosaidia ubunifu wa ndani katika hatua zote, kuanzia wazo hadi biashara.
e) Vyuo vikuu vya kiwango cha kimataifa na vituo mahiri vya utafiti vyenye ushirikiano wa karibu na sekta mbalimbali vikishiriki katika utafiti kuanzia ngazi ya msingi ikiwa ni pamoja na tafiti zinazohusu maarifa asilia zikilenga kutoa ufumbuzi wa masuala mbalimbali yanayoikabili jamii.
f) Mfumo thabiti wa ubunifu wenye uwezo wa kubashiri na kulifanya taifa kuwa kinara katika masuala ya ubunifu duniani.

## 5.6 Mageuzi ya Kidijitali

Mageuzi ya dijitali kwa kiasi kikubwa yanaweza kuharakisha mafanikio ya Tanzania kuelekea malengo yake ya 2050 kwa kuboresha ukuaji wa uchumi, utoaji wa huduma, na kukuza ubunifu kupitia teknolojia za dijitali. Aidha, Tanzania inaweza kuongeza ushindani wake katika uga wa teknolojia na kuhakikisha kuwa kuna maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia uamuzi unaotokana na data za utafiti, kupanua ujumuishi wa kifedha, kukuza ujuzi na huduma za dijitali, pamoja na kutumia teknolojia mpya zinazoibukia.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika teknolojia za dijitali, hususani kupitia kuongezeka kwa matumizi ya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi, upanuzi wa upatikanaji wa intaneti yenye kasi, na serikali mtandao inayoboresha utoaji wa huduma. Aidha,

teknolojia za dijitali zimeleta mabadiliko katika sekta za fedha, afya, elimu, na kilimo kwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma zikichagizwa zaidi na uunganishaji wa intaneti. Kuibuka kwa vituo na kampuni changa zinazojihusisha na masuala ya teknolojia vinavyosaidiwa na serikali kunadhihirisha dhamira ya dhati ya nchi kutumia teknolojia ya dijitali kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Aidha, jitihada kubwa zimefanyika katika usimamizi wa data kwa kutambua umuhimu wake katika kufanya uamuzi unaozingatia taarifa sahihi, utoaji mzuri wa huduma, na maendeleo kwa ujumla. Jitihada hizi zinajumuisha kuanzishwa kwa mifumo ya kitaasisi ya usimamizi wa data na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya data, kama vile uanzishwaji wa vituo vya kuhifadhi taarifa.

Pamoja na mafanikio haya, maendeleo ya dijitali nchini yanakabiliwa na changamoto kama vile miundombinu duni, vitisho vya usalama wa mtandao, gharama kubwa, upungufu wa ujuzi, na vikwazo vinavyotokana na mifumo ya udhibiti vinavyokwamisha utekelezaji na usambazaji wa teknolojia. Aidha, tofauti za upatikanaji, wasiwasi kuhusu faragha ya taarifa na matumizi mabaya ya teknolojia, ugumu katika kupokea mabadiliko, uwekezaji wa kifedha hususani kwenye teknolojia zinazoibukia kama vile akili unde, *blockchain*, *internet of things* na mifumo duni ya kisera vinakwamisha maendeleo ya kidijitali.

**Matarajio**

a) Jamii inayokuza uelewa wa kidijitali na kutumia mbinu salama za dijitali na teknolojia zinazoibuka ili kutumia fursa, kushughulikia vitisho, kuboresha ufanisi, na kuleta mabadiliko.
b) Kitovu cha kikanda cha maendeleo ya teknolojia ambacho kinatumia teknolojia zinazoibukia ikiwa ni pamoja na akili unde, *blockchain*, *internet of things* ili kuchochea ubunifu, maendeleo ya uchumi, na kuimarisha ushindani wa kimataifa huku ikizingatia maadili na uwajibikaji katika teknolojia hizo.
c) Upatikanaji wa huduma za mawasiliano za uhakika na za gharama nafuu pamoja na intaneti yenye kasi kote nchini.
d) Kuwa na mfumo madhubuti, jumuishi wa utoaji wa takwimu za ubora na upatikanaji wa data za mara kwa mara, ambazo zimejumuishwa katika mifumo ya kitaifa na ya sekta ili kusaidia ufuatiliaji, tathmini, na maboresho ya programu za maendeleo.
e) Biashara ya data iliyopanuka kwa kiwango kikubwa ili kuongeza thamani ya kiuchumi, kukuza mifano mipya ya biashara, na kuzalisha ajira
f) Kitovu cha kikanda kinachoongoza kwa uundaji wa maudhui ya digitali, kwa matumizi ya ndani na nje.

# SEKTA ZA KIMAGEUZI

## 6.1 Utangulizi

Sekta zinazochochea mabadiliko ni muhimu katika kufikia Dira ya 2050, zikitoa msukumo wa maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na mazingira yanayoendana na malengo ya kitaifa ya muda mrefu. Sekta hizi zina uwezo mkubwa wa ukuaji, kutoa fursa za ajira, na ubunifu, na kuchochea shughuli za uzalishaji na huduma ambazo ni muhimu kwa masoko ya ndani na nje. Pamoja na utajiri wake wa rasilimali na fursa, Tanzania, ipo katika nafasi nzuri ya kutumia kikamilfu fursa zitokanazo na sekta hizi na hivyo, kuongeza ubora wa maisha na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi.

Katika muktadha huu, Dira ya 2050 inazipa kipaumbele sekta zilizo na uwezo mkubwa wa kuongoza mageuzi ya kijamii na kiuchumi ili kuchochea ukuaji wa uchumi katika miongo ijayo. Sekta hizi zimegawanywa katika makundi matatu: *Sekta chochezi* ambazo huchochea kasi ya ukuaji wa haraka wa uchumi kupitia mauzo ya nje ya thamani kubwa au bidhaa zinazoweza kuuzwa; *Sekta za ajira*, ambazo zinazalisha fursa nyingi za ajira jambo ambalo ni muhimu kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu; na *sekta unganishi* ambazo huwezesha upatikanaji wa rasilimali muhimu, huduma, na miundombinu ili kuimarisha uzalishaji na kuunganishwa kwa sekta zingine. Sekta hizi kwa pamoja zinawezesha ugawaji mzuri wa rasilimali, mpangilio wa sera za kimkakati, na kuchangia kwa ufanisi matarajio ya Dira ya 2050, ikiwa ni pamoja na kupunguza umaskini, kuongeza ubora wa maisha, na uendelevu wa mazingira.

Dira inasisitiza uwekaji vipaumbele kwa uwiano wa sekta ili kuwezesha uchumi endelevu na ukuaji mseto unaohusisha sekta nyingi na fursa kubwa za ajira. Kwa kutumia vigezo maalum vya utambuzi wa sekta zenye matokeo makubwa, Dira ya 2050 inahakikisha umuhimu wa uendelevu wake, kuendana na vipaumbele vinavyobadilika na kuhakikisha uhimilivu wa muda mrefu katika mazingira ya kuyumba kwa soko la dunia. Uwezo wa kubadilika unaiwezesha Tanzania kukabiliana na changamoto na na kutumia fursa zilizopo kwa mustakabali wa ustawi na uchumi jumuishi , na hivyo kuwa katika nafasi nzuri

## 6.2 Lengo

Kuanzisha mfumo thabiti wa kimkakati wa kutambua na kuibua sekta za mageuzi zinazoendana na malengo ya Dira ya 2050, ili kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia ukuaji endelevu, uzalishaji wa ajira, na ubunifu

## 6.3 Vigezo vya Uchaguzi wa Sekta

Kwa kutambua kwamba vipaumbele vya leo vinaweza kubadilika katika kukabiliana na mabadiliko ya mienendo ya kitaifa na kimataifa, upatikanaji wa rasilimali, ukuaji wa idadi ya watu, na maendeleo makubwa katika sayansi na teknolojia, Dira ya 2050 inaweka vigezo vinavyoweza kubadilika vya kuchagua sekta zenye usawa, zenye athari kubwa na uwezo wa kuendesha ukuaji wa uchumi tofauti, kutengeneza ajira, na uhusiano wa sekta. Njia hii inalinda umuhimu wa Dira na uwiano na maendeleo ya baadaye, kukuza ujasiri na uendelevu katika uchumi wa Tanzania.

i. **Uwezo wa kuzalisha ajira:** Sekta yenye fursa ya kuzalisha ajira nyingi ikiwa na uwezo wa kuchochea ajira za moja kwa moja na ajira ya ziada katika tasnia zilizounganishwa. Kigezo hiki kinatathmini jinsi ongezeko la ukuaji wa ajira ndani ya sekta, ukinufaisha sekta nyingine na uhusiano wake ndani ya soko la ajira.
ii. **Mauzo ya nje**: Sekta yenye mchango mkubwa wa mauzo au huduma nje ya nchi. Uwezo huu wa kuuza nje unapaswa kuimarishwa na minyororo ya usambazaji yenye ufanisi na endelevu ili kuongeza ushindani wa kimataifa na ustahimilivu wa kiuchumi.
iii. **Uwezo wa kuchochea ukuaji wa sekta zingine:** Sekta yenye uhusiano thabiti na sekta zingine katika kuchochea uzalishaji wa malighafi na huduma, usambazaji wa bidhaa na huduma za ndani na nje. Uhusiano huo unawezesha kuwa na mnyororo wa thamani unaohusisha sekta mbalimbali katika kuchangia ukuaji wa uchumi.

## 6.4 Sekta za Kimkakati

### 6.4.1 Kilimo: Mazao, Mifugo, Uvuvi, na Misitu

Umuhimu wa Sekta ya kilimo kama kipaumbele cha Dira ya 2050 unatokana na uwezo mkubwa wa sekta hiyo kwenye mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Kwa sasa, Kilimo kinachangia asilimia 26.7 ya Pato la Taifa, kinaajiri asilimia 65 ya nguvukazi, na kinazalisha asilimia 30 ya mapato ya nje, hii inadhihirisha nafasi yake katika ukuaji wa uchumi na usalama wa maisha. Sekta hii, ambayo inajumuisha mazao, mifugo, uvuvi, na misitu, kimsingi inahudumia soko la ndani, ambapo wakulima huzalisha chakula kwa matumizi ya hapa nchini, huku uuzaji wa mazao nje ukiwa ni wa kiwango kidogo. Ongezeko la uzalishaji wa chakula kwa ajili ya kuuza nje, kutaiwezesha Tanzania kutumia vyema fursa ya ongezeko la mahitaji ya chakula duniani, kuongeza fursa za upatikanaji wa masoko na kukuza biashara. Ili mabadiliko hayo yatokee, kunahitajika mageuzi makubwa kwenye kuongeza tija na uanzishwaji wa mifumo saidizi ya masoko ili kuvutia uwekezaji, hasa kutoka kwa wakulima wadogo.

Kufanya mageuzi katika tasnia zote hizi kutahitaji kuboresha tija kupitia teknolojia za kisasa kama vile kilimo cha kisasa, uboreshaji wa miundombinu, na upatikanaji wa soko la uhakika. Katika tasnia ya mazao, uendelezaji wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji kutaongeza mavuno na kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Kwa tasnia ya *mifugo*, kuimarisha huduma za afya ya wanyama na kutumia njia endelevu za malisho kutawezesha ongezeko la tija na ubora wa mazao kwa masoko ya ndani na nje. Sekta ya *Uvuvi* inaweza kufaidika ikiwa kutakuwa na udhibiti wa kisayansi wa uvuvi usio endelevu, na uboreshaji wa miundombinu ili kufikia viwango vya kimataifa, Kwa upande mwingine usimamizi endelevu wa misitu utasaidia kuwianisha ukuaji na uhifadhi wa mazingira.

Kuwapo kwa ardhi kubwa yenye rutuba, hali ya hewa tofauti katika tekolojia za kilimo, na rasilimali nyingi za asili, kutaiwezesha Tanzania kujiimarisha kama mzalishaji mkuu wa chakula katika kanda hii. Afua za kimkakati katika kilimobiasharamsisitizo ukiwa katika mazao muhimu kama vile korosho, kahawa, chai, miwa, na uuzaji nje wa mboga na matunda zina uwezo mkubwa katika kuleta mageuzi ya kilimo.

Uongezaji wa thamani ya mazao utawezesha kuongeza kipato, kuzalisha na kuinua hadhi ya Tanzania katika soko la kimataifa la mazo na bidhaa za kilimo. Sera mahususi na uwekezaji vitahakikisha kuwa kilimo kinachochea ukuaji jumuishi na endelevu, na kukifanya kuwa nguzo mojawapo katika Dira ya 2050 inayohusu uhimilivu na Uchumi shindani. Tanzania inaweza kuchukua sehemu kubwa ya mnyororo wa thamani wa kimataifa, kuboresha ushindani wa bidhaa za nje, na kuhakikisha utulivu wa kiuchumi wa muda mrefu kwa kubadilisha mazao ghafi ya kilimo kuwa bidhaa zenye thamani kubwa.

### 6.4.2 Huduma kwa Watumiaji

Sekta hii, inajumuisha biashara za rejareja, utalii, ukarimu na sekta nyingine zinazohusiana nazo ambazo zinaajiri nguvukazi kubwa hususani katika maeneo ya mjini. Sekta hii ni ya pili kwa uzalishaji wa ajra baada ya kilimo. Hivyo, ni sekta muhimu ya kimkakati katika kufikia malengo ya Dira ya 2050. Ingawa sekta hii inaonekana kuwa na tija ndogo kuliko sekta ya kilimo, uhalisia ni kwamba ni sekta yenye tija kubwa na ina mchango mkubwa katika ufanisi wa kiuchumi.

Kupanua na kurasimisha huduma hizo kupitia mageuzi ya kimfumo ikijumuisha kiteknolojia kunaweza kuongeza ukuaji tija na uhimilivui wa kiuchumi. Kubadilisha biashara ndogo zisizo rasmi kuwa za kati na rasmi, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa mitaji na elimu ya biashara, kutachangia kuongeza ubora na ufanisi wa huduma na ufanisi. Hii inaoana na malengo ya Dira ya 2050 ya ukuaji endelevu wa miji na

kupunguza umaskini, kuwezesha sekta hiyo kuwa sehemu ya hatua ya Tanzania kuelekea uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu.

### 6.4.3 Utalii

Suala la sekta ya utalii kuwa moja ya vipaumbele katika Dira ya 2050 ni jambo lisiloepukika kwani imedhihirisha kuwa kichocheo muhimu katika ukuaji wa kijamii na kiuchumi. Kama moja ya sekta muhimu za "kichocheo" kwa Tanzania, katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, utalii umehangia takriban asilimia 17 ya Pato la Taifa. Kwa kuzingatia ongezeko la watalii ambapo mwaka 2023 kulikuwa watalii takriban milioni 1.8, sekta hii inasaidia ukuaji wa sekta nyingine kama vile usafirishaji, ukarimu, na biashara za rejareja, huku ikichochea maendeleo ya uchumi wa ndani.

Ili kuendeleza na kupanua manufaa haya, ni muhimu kushughulikia upungufu katika miundombinu, malazi, gharama za usafiri, na wigo mdogo wa bidhaa za utalii. Uhusiano wa utalii, maliasili na rasilimali za utamaduni hufanya uhifadhi wa mazingira kuwa muhimu kwa ukuaji wake wa muda mrefu. Juhudi za uhifadhi zinahakikisha kuwa vivutio maarufu vya Tanzania kama vile Zanzibar, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Ngorongoro na Mlima Kilimanjaro vinaendelea kuvutia watalii.

Utalii wa Tanzania wa wanyamapori unachangia zaidi ya asilimia 80, juhudi za hivi karibuni za kupanua bidhaa za utalii zimelenga kukuza maeneo ya urithi wa kitamaduni, mipango ya utalii wa mazingira katika maeneo kama misitu ya asili, utalii wa jamii na katika maeneo ambayo hayatembelewi mara kwa mara kama Ruaha na Selous kusini mwa Tanzania. Uwekezaji pia unafanywa katika bidhaa nyingine zinazohusiana na utalii kama vile mikutano, makongamano, na utalii wa maonesho na miundombinu ya utalii wa meli, vinachangia pia kukuza uchumi wa ndani kutokana kuongezeka kwa mahitaji ya huduma na nyenzo mbalimbali. Juhudi za kuimarisha vituo vya mikutano na kuitangaza Tanzania kama kituo cha mikutano zinatarajiwa kuongeza idadi na siku za wageni na kukaa nchi.

Vile vile, sekta ya utalii wa meli za kitalii inaendelezwa kwa kutumia ukanda mrefu wa pwani ya Tanzania wenye uzuri wa asili. Upanuzi wa vituo vya bandari na uendelezaji wa safari za kitalii ambazo ni pamoja na vituo vya Zanzibar, Dar es Salaam, na vivutio vingine vya pwani vinalenga kuvutia watalii wengi zaidi, na hivyo kuongeza mapato kwa wafanyabiashara na jamii za wenyeji. Aidha, juhudi za kutangaza utalii kimataifa zinaendelea kwa kuelezea utajiri wa urithi wa utamaduni wa nchi na vivutio mbalimbali, kuwavutia watalii wa kimataifa kwa maeneo zaidi ya yale ya asili. Utekelezaji wa mikakati ya kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta za burudani, michezo na malazi ni muhimu ili kuimarisha miundombinu ya utalii ya Tanzania. Kwa kuwa na utalii wa aina mbalimbali unaozingatia uwezo wa eneo husika, sekta hii itakuwa himilivu na hivyo

kuwezesha uhifadhi wa urithi wa utamaduni na mazingira, kuchangia ukuaji wa uchumi na kuboresha viwango vya maisha kwa Watanzania.

### 6.4.4 Madini

Tanzania inapaswa kuweka kipaumbele katika kuyaongezea madini thamani ikizingatia uwezo wa sekta hiyo katika ukuaji wa Uchumi. Kwa kihistoria, uchimbaji madini umekuwa kichocheo muhimu katika ukuaji wa wa kiuchumi, hasa kuanzia mwaka 2000 hadi 2014, hivyo, kuiweka Tanzania kuwa miongoni mwa nchi ambazo uchumi ulikua kwa kasi zaidi katika kipindi hicho. Ingawa ukuaji huu baadaye unatarajiwa kuongezeka kwa kuongeza madini mengine tofauti na dhahabu, sekta hii inabaki kuwa na fursa kubwa kutokana uhifadhi wa madini ya kimkakati kama vile grafiti, lithiamu, urani, na madini ambayo ni adimu. Madini haya yana muhimu katika mabadiliko ya nishati ya kimataifa na maendeleo ya kiteknolojia, hivyo kuongezeka kwa thamani yake katika soko la kimataifa.

Mchango wa sekta ya madini ambayo kwa sasa ni asilimia 9 ya Pato la Taifa, unaweza kuongezeka ikiwa jitihada zaidi zitaelekezwa katika uongezaji wa thamani. Ukuzaji wa uchakataji madini na shughuli husiani kutasaidia kuongeza uzalishaji wa ajira, mapato ya fedha za kigeni, na kuwezesha uhawilishaji wa teknolojia, huku ukichangia ukuaji endelevu wa sekta hiyo. Mikakati hii inawiana na malengo ya kitaifa ya kuvutia uwekezaji, kuwezesha upatikanaji wa mitaji, kuboresha miundombinu, na kukuza ushirikiano kati ya serikali, jamii, na sekta binafsi. Kuimarisha taratibu za kimazingira, ushirikishwaji wa jamii, na kuboresha shughuli za uchimbaji madini kwa kutumia teknolojia za kisasa na ukuzaji wa ujuzi ni masuala muhimu kufikia malengo haya.

Kutilia mkazo ongezeko la thamani katika sekta madini kutaimarisha nafasi ya Tanzania katika mchakato wa ugavi wa madini wa kimataifa, kukuza ukuaji jumuishi katika sekta , na kuhakikisha kuwa rasilimali hizi zinachochea mabadiliko yenye tija ya kijamii na kiuchumi. Mkazo huu wa kimkakati ni muhimu katika malengo ya Dira ya 2050 ya kujenga uchumi anwai, unaoweza kuhimili mabadiliko, kuongeza utajiri wa rasilimali, na kuimarisha maendeleo endelevu na utulivu wa kiuchumi wa muda mrefu.

### 6.4.5 Uzalishaji Viwandani

Kuipa kipaumbele sekta ya uzalishaji viwandani ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na uchumi mseto ifikapo mwaka 2050. Manufaa ya sekta hii hayaishii tu katika mchango wake wa sasa wa asilimia 8.1 kwenye Pato la Taifa na ukuaji wa hivi karibuni wa asilimia 8 kwa mwaka bali sekta hii ina uwezo wa kipekee wa kuchangia ukuaji wa sekta zingine, na kujenga uchumi wenye nguvu. Maeneo muhimu, kama vile usindikaji wa mazao ya kilimo, chakula na vinywaji, na vifaa vya ujenzi, vina uwezo mkubwa

kutokana na uwezo wake wa kuongeza thamani ya ndani, kupunguza utegemezi wa uagizaji, na kuongeza mauzo ya nje, na hivyo kuimarisha usawa wa biashara na kuzalisha fedha za kigeni.

Sekta hii pia ina mchango mkubwa katika kuzalisha ajira kwa watu wenye ujuzi tofauti wakiwamo wenye ujuzi wa chini na ujuzi wa juu. Hii ni fursa muhimu sana kwa kuzingatia kuwa idadi ya vijana wa Tanzania inakua na itahitaji njia endelevu za ajira. Kadiri sekta hii inavyopanuka, inaweza kuunganishwa na sekta zingine za mageuzi kama kilimo, madini, na ujenzi na kujenga mnyororo wa uhusiano. Kwa mfano, usindikaji wa mazao ya kilimo unaweza kutumia mazao ya kilimo yanayozalishwa ndani, kuongeza kipato kwa wakulima na kuendesha mahitaji katika maeneo ya vijijini.

Kimkakati, Tanzania inatekeleza juhudi zilizoratibiwa zinazolenga mageuzi ya udhibiti na miundo iliyoundwa ili kuongeza ubunifu, kuboresha ufanisi, na kuimarisha ushindani wa sekta. Serikali ya Tanzania ina mpango wa kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika vyanzo vya uhakika vya nishati, kwa lengo la kuongeza matumizi ya nishati kwa kila mtu kutoka wastani wa sasa wa 120 kWh hadi 600 kWh. Lengo hili kabambe litasaidiwa na uwekezaji thabiti katika mchanganyiko wa nishati safi, ikiwa ni pamoja na umeme wa maji, nishati ya jua, upepo, na jotoardhi. Mathalani, mradi wa umeme wa maji wa Mwalimu Nyerere unatarajiwa kuzalisha MW 2,115 kwa mwaka, kuimarisha gridi ya taifa na kuimarisha upatikanaji wa nishati kwa ujumla. Aidha, serikali inalenga kupunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 16 hadi chini ya asilimia 10 kwa kuboresha mifumo ya usambazaji umeme. Mipango hii ya kimkakati, pamoja na kuimarisha miundombinu ya usafiri, itajenga mazingira ya nishati ya kuaminika ambayo inasaidia ukuaji wa viwanda.

Hata hivyo, kuweza kutumia uwezo huu kunahitaji kukabiliana na changamoto, ikiwa ni pamoja na changamoto ya miundombinu, ugumu wa udhibiti, na upatikanaji wa fedha za riba nafuu. Jitihada zilizoratibiwa kuelekea uthabiti wa sera, maendeleo ya ujuzi, wafanyakazi wanaobadilika, soko, nguvu ya kuaminika na miundombinu ya usafirishaji itaweka mazingira ambayo yatavutia wawekezaji wa ndani na wa kigeni. Kushughulikia vikwazo hivi kunaweza kuimarisha uzalishaji na ufanisi wa viwanda, na kuiwezesha Tanzania kuwa na ushindani zaidi katika masoko ya kikanda na kimataifa.

### 6.4.6 Huduma za Fedha

Sekta ya huduma za fedha ni muhimu katika utekelezaji wa Dira ya 2050, kutokana na uwezo wake wa kuchochea ukuaji wa kiuchumi, kuimarisha ujumuishaji wa kifedha, na kuongeza uhimilivu wa kiuchumi. Ukuaji wa huduma za kibenki kwa njia simu na huduma ndogo ndogo za kifedha zinazowafikia Watanzania zaidi ya milioni 20, umeifanya sekta hii kuweka msingi wa mageuzi makubwa ya kiuchumi. Uimarishaji wa

sekta hii utakuza uwekezaji, kuimarisha biashara ndogo na za kati, kuzalisha ajira, na kuimarisha usawa, hasa katika maeneo ambayo huduma za kifedha bado ni changamoto. Kuongeza ujumuishaji pia kutahamasisha uwekaji wa akiba na uwekezaji kwa viwango vya mtu binafsi na biashara, kuchochea kukusanya mtaji na kukuza ushiriki wa kiuchumi.

Aidha, sekta imara ya huduma za fedha inaweza kuharakisha maendeleo ya kiteknolojia na miundombinu, ambayo ni muhimu katika kuboresha uchumi wa Tanzania. Kupanua miundombinu ya benki ya kidijitali na simu kunaweza kuongeza upatikanaji, ujuzi wa kifedha, na kukuza ukuaji wa sekta kama vile, kilimo na viwanda, ambapo upatikanaji wa mtaji ni muhimu kwa shughuli za kuongeza uzalishaji. Ili kunufaika na maendeleo haya, mageuzi ya kimfumo katika miundombinu bora ya dijitali, na mkopo wa gharama nafuu ni muhimu katika kujenga uhimilivu na kuiunganisha sekta hiyo na malengo ya Dira ya 2050 ya uchumi anwai, jumuishi, na endelevu. Hatua mahususi za kisera katika maeneo haya zitahakikisha kuwa sekta hii inawezesha ukuaji wa Uchumi na kuchangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania.

### 6.4.7 Ardhi

Sekta ya ardhi ni muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Inachangia katika pato ya taifa, kuwa kiungo wezeshi kwa sekta nyingine za uzalishaji, na hivyo kuongeza thamani na mahitaji ya ardhi nchini. Sekta hizo ni pamoja viwanda, kilimo, mifugo, miundombinu, na maendeleo ya mali zisizohamishika.

Shughuli kama vile upangaji wa miji na na vijiji, upimaji wa ardhi, uchoraji wa ramani, upatikanaji wa ardhi, usajili na umiliki wa ardhi na shughuli zinazohuaiana nazo, tathmini ya ardhi na majengo, ujenzi wa nyumba bora, maendeleo ya mali isiyohamishikaa, usimamizi wa rekodi za ardhi, ukusanyaji na usimamizi wa mapato yatokanayo na ardhi, na utatuzi wa migogoro ya ardhi vinasimamiwa kikamilifu.

Kimsingi ardhi kama mtaji inaweza kuuzwa na kununuliwa kama bidhaa nyingine yoyote, hivyo, inahitaji mfumo madhubuti wa usimamizi na uratibu katika uendelezaji wake. Hali ambayo inaweza kusaidia kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, sekta hii kuwa moja ya vipaumbele katika Dira ya 2050 kunaongeza ya mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi.

### 6.4.8 Ujenzi na Mali isiyohamishika

Kuweka sekta za ujenzi na mali isiyohamishika ndani ya Dira ya 2050 kunatoa njia ya mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi. Sekta hizi kwa pamoja zinachangia

asilimia 16 hadi 19 ya Pato la Taifa, ikisisitiza nafasi yake muhimu ya kuchangia ukuaji wa uchumi. Sekta ya ujenzi, ambayo ilikuwa kwa wastani wa asilimia 9 kwa mwaka baina ya mwaka 2015 hadi 2020, imechochewa na miradi mikubwa ya miundombinu kama reli ya kiwango cha kimataifa na maboresho mengine ya miundombinu. Mbali na ujenzi, sekta hii pia inachangia ukuaji wa biashara zikiwamo za rejareja, kukidhi ongezeko la mahitaji ya maghala na nyenzo za lojistiki kadiri Tanzania inavyoojiweka kwenye nafasi nzuri ya kushiriki katika ushindani wa biashara ya kikanda inayoongezeka.

Mali isiyohamishika imeonyesha ukuaji thabiti kufikia asilimia 3 hadi 4 ya Pato la Taifa, inayotokana na ongezeko la mahitaji ya majengo kwa ajili ya makazi, biashara, na viwanda. Ongezeko hilo linachangiwa na sababu mbalimbali kama vile ukuaji wa miji na ongezeko la watu, ongezeko la watu wenye kipato cha kati, maendeleo ya miundombinu, utalii na ukuaji wa sekta za ukarimu, sera na mipango ya serikali ya ujenzi wa nyumba, upatikanaji wa mikopo ya ujenzi wa nyumba na ongezeko la uwekezaji kutoka nje.

Uendelezaji wa mali isiyohamishika inalenga changamoto za ukuaji wa miji na mahitaji ya nyumba. Sekta hii ni kichocheo katika maendeleo kwenye nyanja mbalimbali. Kadiri mahitaji ya majengo kwa ajili ya makazi, biashara na viwanda yanavyoongezeka hususani katika miji inayokuwa kwa kasi, sekta ya mali isiyohamishika inachochea maendeleo katika sekta nyingine kama vile ujenzi, fedha na usimamizi wa majengo.

Uendelezaji wa mali isiyohamishika ni muhimu katika kutatua changamoto ya upungufu wa nyumba na kuchangia katika ukuaji jumuishi wa miji ambayo ni muhimu katika kukidhi mahitaji ya makazi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu. Aidha, sekta hii inavutia uwekezaji wa ndani na nje na kuchangia katika kujenga uchumi imara unaozalisha utajiri.

Kwa kupanua miundombinu ya mali isiyohamishika Tanzania inaweza kuboresha mazingira yake ya biashara na kuifanya ivutie wawekezaji kutoka nje na wakati huohuo ikichangia kuboresha maisha ya wananchi wake kupitia uboreshaji wa makazi na maeneo mengine ya umma.

Ili Tanzania inufaike kikamilifu na sekta za ujenzi na mali isiyohamishika, itahitaji kuanzisha mfumo wa kisheria ulio imara, wa wazi na wenye ufanisi. Aidha, changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja mipango miji isiyokidhi mahitaji ya watu wote inapaswa kushughulikwa. Kwa sekta ya ujenzi, gharama kubwa za ujenzi ni miongoni mwa changamoto zinazopaswa kushughulikiwa. Uwekezaji wa kimkakati katika kuimarisha ujuzi, mageuzi ya kisera na ushirikiano na sekta binafsi vinaweza kuchangia katika

kuziinua sekta kama ilivyolengwa katika Dira ya 2050 inayohusisha ukuaji endelevu wa miji na miundombinu himilivu.

### 6.4.9 Uchumi wa Bluu

Uchumi wa bluu wa Tanzania unazidi kutambuliwa kwa uwezo wake wa kuendesha ukuaji endelevu wa uchumi kupitia sekta kama vile utalii wa baharini, rasilimali za maji, uvuvi endelevu, na nishati ya pwani. Nchi hii ina zaidi ya kilomita 1,400 za pwani na Eneo la Uchumi la kipekee la takriban kilomita za mraba 223,000, kusaidia uvuvi tofauti na maisha ya baharini. Sekta ya uvuvi inaajiri watu karibu milioni 2.5 na inachangia asilimia 1.5 kwa Pato la Taifa.

Sehemu muhimu ya ukuaji huu ni maendeleo ya gesi asilia iliyosafishwa (LNG), na makadirio yanaonyesha zaidi ya futi za ujazo trilioni 57 za akiba ya gesi asilia katika ukanda wa pwani huko Lindi na Mtwara. Kituo cha kuuza nje cha LNG kinachopendekezwa cha dola bilioni 42 mkoani Lindi kinatarajiwa kuzalisha tani milioni 10 kwa mwaka. Kituo hiki kitajengwa karibu na kongani za viwanda mahususi kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mbolea. Ujenzi unatarajiwa kuzalisha maelfu ya ajira na kuimarisha usalama wa nishati na kuwezesha upatikanaji wa nishati safi ikilinganishwa na makaa ya mawe na mafuta. Mipango ya kimkakati ya Tanzania ya maendeleo ya LNG inalenga kuvutia uwekezaji mkubwa na kuanzisha mfumo thabiti wa udhibiti na kuifanya Tanzania kuwa kituo cha kikanda cha uzalishaji wa nishati huku ikihakikisha kwamba faida za LNG zinawanufaisha wananchi wote.

Mbali na LNG, maendeleo ya miundombinu ya usafirishaji na bandari ni muhimu kwa matarajio ya kiuchumi ya Tanzania. Serikali inapanga kuwekeza takriban dola bilioni 1.5 katika uboreshaji wa bandari, kuimarisha uwezo wa Bandari ya Dar es Salam kushughulikia uingizaji wa tani zaidi ya milioni 30 ifikapo mwaka 2025 na kuendeleza bandari ya Bagamoyo ambayo inatazamiwa kuwa moja ya uwezekaji wa kimkakati katika kanda hii. Upanuzi huu utaboresha kwa kiasi kikubwa usafirishaji, kupunguza muda na gharama za usafirishaji, na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha ushindani wa biashara katika ukanda huu.

Aidha, upanuzi wa umeme wa maji ni lengo lingine la kimkakati kwa maendeleo endelevu. Pamoja na uwezo wa sasa wa MW 561, serikali inakusudia kuongeza umeme wa maji kwa kutumia bwawa la Mwalimu Nyerere ambao peke yake inatarajia kuzalisha MW 2,115 kwa mwaka. Upanuzi huu hautakidhi tu mahitaji ya nishati ya ndani bali pia kutoa nishati ya ziada kwa ajili ya kuuza nje, kuchangia mapato ya taifa na usalama wa nishati ya kikanda. Mipango hii ya kimkakati kwa pamoja inasaidia kuunganisha rasilimali za uchumi wa bluu na kuchangia kwa kiasi ukuaji wa Pato la

Taifa, uzalishaji wa ajira, kuimarishaji usalama wa nishati na kuifanya Tanzania kuwa kinara wa kiuchumi kikanda.

### 6.4.10 Michezo na Sanaa ya Ubunifu

Kuweka michezo na sanaa za ubunifu kama sekta ya kipaumbele ndani ya Dira ya 2050 ni muhimu katika kuunganisha uwezo wa kijamii na kiuchumi kwa idadi kubwa ya vijana nchini, ambayo inajumuisha takriban asilimia 75 ya idadi ya watu wote. Sekta ya michezo na sanaa ya ubunifu inatoa fursa kubwa kwa ukuaji wa uchumi, mshikamano wa kijamii, na uwezeshaji wa vijana, kutoa njia tofauti za ajira, maendeleo ya ujuzi, na kuzalisha mapato. Sekta hizi zinashirikisha vijana wenye nguvu, na kutengeneza njia za kuchangia uchumi na kuimarisha utambulisho wa kitaifa. Kwa kukuza vipaji na kuweka mifumo thabiti, Tanzania inaweza kufungua uwezo wa ubunifu na ujasiriamali wa vijana wake, kuendesha mabadiliko ya kiuchumi ya muda mrefu.

Maendeleo ya michezo na sanaa za ubunifu nchini Tanzania yanahitaji msaada wa kimkakati wa serikali katika sekta ndogo kama riadha, mpira wa miguu, muziki, filamu, na sanaa za dijitali. Serikali ina jukumu muhimu katika kuanzisha sera, kutenga rasilimali kwa ajili ya miundombinu, na kujenga taasisi zinazokuza ukuaji katika sekta hizi. Uwekezaji katika miundombinu ya michezo, vifaa vya mafunzo, na vyuo vya michezo vinaweza kukuza vipaji kutoka umri mdogo na kuiweka Tanzania kama kitovu cha michezo cha kikanda. Katika sanaa ya ubunifu, mipango ya serikali ya kukuza elimu, kuboresha upatikanaji wa teknolojia, na kulinda haki za milikibunifu inaweza kuongeza vipaji vya ndani na kufungua milango kwa masoko ya kimataifa. Majukwaa ya dijitali yanayosaidiwa na serikali yataruhusu wabunifu kufikia hadhira pana, na kuzalisha mapato kupitia mauzo ya nje ya dijitali na utalii wa kitamaduni. Kuwianisha sekta za michezo na ubunifu wa sanaa na malengo mapana ya maendeleo ya Tanzania kunahitaji mazingira mazuri ya udhibiti, kwani sekta hizi zinaweza kuchangia pato la taifa, kutengeneza ajira na utalii. Mipango katika utalii wa michezo, ushirikiano wa kimataifa, mipango ya maendeleo ya vijana, na majukwaa ya kuonyesha vipaji inaweza kuongeza ukuaji wa uchumi, kukuza ubunifu, na kujenga ufahari wa kitaifa. Kupitia juhudi hizi, sanaa za michezo na ubunifu zinaweza kuwa sekta za muhimu za mageuzi katika kufikia Dira ya Taifa ya 2050 na kujenga uchumi imara na ushindani.

# UTEKELEZAJI WA DIRA

Ili kutekeleza Dira ya Tanzania 2050 kwa ufanisi, itakuwa muhimu kuweka vipaumbele vya kimkakati, kuzingatia mbinu zinazoleta matokeo; na kuwa na mifumo thabiti ya uwajibikaji na nidhamu ya utekelezaji. Kama mwongozo mkuu wa taifa kwa miaka 25 ijayo, ni sharti Dira hii ifungamanishwe na sera zote za kisekta, mipango na programu ili kuzuia kuwepo kwa utitiri wa dira ndogo ndogo za kisekta.

### 7.1 Uwekaji wa Vipaumbele vya kimkakati

Kutokana na rasilimali chache zilizopo ikilinganishwa malengo mapana ya Dira 2050, ni muhimu kuweka wazi vipaumbele vya nchi. Kwa mnasaba huo, Dira imebainisha maeneo matatu ya kipaumbele: (i) Msingi Mkuu wa Utawala Bora, Amani, Usalama na Utulivu; (ii) Nguzo tatu ambazo ni Uchumi wenye nguvu, Jumuishi na Shindani; Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii; na Uhifadhi wa Mazingira na Uhimilivu wa Mabadiliko ya tabianchi na (iii) Vichocheo vinne vinavyoendesha Dira ambazo ni Usafirishaji Fungamani;, Sayansi na Teknolojia; Utafiti na Maendeleo; na Mageuzi ya Kidijitali. Aidha, Dira imebainisha vigezo muhimu vya kuzingatia wakati wa kuchagua sekta za kimageuzi zitakazochochea ukuaji wa kiuchumi na kijamii.

### 7.2 Utekelezaji wa Dira

Dira 2050 itatekelezwa kupitia mipango ya maendeleo ya miaka mitano-mitano inayotokana na mpango elekezi wa miaka 25. Mipango hii ya miaka mitano-mitano itaongozwa na vipaumbele mahususi vitakavyozingatiwa katika utekelezaji wa kila mpango husika. Kwa upande mwingine, mipango hiyo itagawanyika katika vipindi vya utekelezaji vya mwaka mmoja mmoja.

#### a. Mikakati ya Kisayansi ya Utekelezaji

Ili Dira ya 2050 itekelezwe kwa ufanisi, ni lazima kuwa na mikakati iliyoandaliwa kisayansi kwa kutumia data, uchambuzi wa mwenendo wa idadi ya watu; mahitaji ya rasilimali, na kuzingatia vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

#### b. Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji, tathmini na uzoefu ni muhimu katika kutekeleza Dira 2050, kwani inapima hatua zinazofikiwa, uwajibikaji na uwezo wa kufanya mabadiliko.

Ili kuimarisha ufuatiliaji na tathmini, ni muhimu kuwa na vigezo vya kupima ufanisi kwa kila sekta. Vigezo hivi vinawezesha ufuatiliaji sahihi wa hatua zilizofikiwa, kuonesha mafanikio na kutambua maeneo yanayohitaji kuboreshwa malengo ya Dira 2050.

Pamoja na ufuatiliaji na tathmini, ni muhimu kuwa na mfumo utakaotoa motisha kwa watendaji na taasisi zinazofanya vizuri, na kuchukua hatua kwa wale ambao hawatimizi wajibu wao ipasavyo. Mfumo huo utakuza utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii na kuimarisha uwajibikaji.

**c. Uratibu na Usimamizi wa Utekelezaji wa Dira 2050**

Utekelezaji madhubuti wa Dira 2050 unahitaji uratibu thabiti na uwiano muafaka wa nafasi ya Serikali na ya sekta binafsi. Tume ya Taifa ya Mipango itakuwa mratibu mkuu wa kuainisha mikakati na rasilimali za kisekta na malengo ya Dira 2050, wakati huo huo ikihakikisha kuna ushirikiano thabiti na wadau wote husika. Njia hii itahamasisha utafutaji wa rasilimali wa pamoja, mawasiliano ya kimkakati na ushiriki mpana wa wadau, kuhakikisha kuwa juhudi zote zinawiana katika kutekeleza malengo ya Dira.